KUHAMASISHA UHIFADHI WA KISWA CHA MISALI ZANZIBAR

# Mwongozo wa elimu ya mazingira kwa walimu wa Kiislamu



Fazlun Khalid na Ali Kh. Thani

2008

Fazlun Khalid na Ali Kh. Thani wameruhusu uchapishaji zaidi wa nakla ya kitabu hiki kwa mtu yeyote ulimwenguni ili kuwezesha waislamu popote walipo kutunza mazingira ya sayari hii kwa ajili ya vizazi vijavyo.

Kimechapwa na
The Islamic Foundation for Ecology and Environmental Sciences
93 Court Road, Balsall Heath
Birmingham B12 9LQ,
England
January 2008

Uchapishaji na usambazaji wa kitabu hiki umefanywa kwa hisani ya taasisi za Muslim Hands ya Nottingham na Islamic Relief ya Birmingham, Uingereza(U.K)

Kitabu hiki kimeingizwa katika mtiririko wa kumbukumbu za vitabu ndani ya Maktaba kuu ya Uingereza
ISBN: 978-0-9534248-2-5

# YALIYOMO


Dibaji ya mwandishi 1

Utangulizi 4

- Kisiwa cha Misali na umuhimu wake 4
- Mradi wa uhifadhi mazingira kwa kuhusisha maadiili ya dini 5
- Uislam na uhifadhi wa mazingira 5
- Jinsi ya kutumia mwongozo huu 11

Somo la kwanza – Tawheed 14

Somo la pili – Khalq 20

Somo la tatu – Mizan 28

Somo la nne – Insan 37

Somo la tano – Fasad 43

Somo la sita – Khalifa 48

Hitimisho 54

Maneno ya mwisho ya mwandishi 56

Baadhi ya hadithi za S.A.W 58

Vitabu rejea 60

Maana ya maneno magumu yaliyotumika 62

Misamiati maarufu inayotumika katika masuala ya Uhifadhi 64

## DIBAJI YA MWANDISHI

Mradi wa elimu ya mazingira wa kisiwa cha Misali ni moja katika jitihada za aina yake ambapo mfumo wa utekelezaji wake ulishirikisha taasisi ya kiislamu na isiyokuwa ya kiislamu katika uwanja wa mazingira. Ushirikiano huu siyo jambo jipya lakini kitu cha mfano ni kule kuchukua ujumbe wa Qur'an na sunna na kuhusisha katika fani ya mazingira ya bahari na hatimaye kuuweka katika matumizi halisi kwa jamii ya kiislamu katika maeneo husika.

Ushirikiano baina ya shirika la kimataifa la CARE (Tanzania) na Taasisi ya Kiislamu inayoshughulikia Ekologia na Sayansi ya Mazingira (IFEES) iliopo nchini Uingereza, umeweka msingi mzuri kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya namna hii sehemu nyengine katika siku za baadae. Jambo la kutia moyo kuhususiana na mradi huu ni kule kupata uungwaji mkono kutoka serikali ya Zanzibar na pamoja na Mufti Mkuu wa Zanzibar yeye binafsi.

Ushiriki wa Taasisi ya Kiislamu inayoshughulikia Ekologia na Sayansi ya Mazingira (IFEES) iliopo nchini Uingereza, ulianza mnamo mwaka 1999. Tunamshukuru Bwana Rob Wild aliyekuwa Mratibu wa Mradi wa Jozani na Ghuba ya Chawaka uliokuwa ukisimamiwa na shirika la CARE Tanzania kwa wakati huo kwa msaada wake mkubwa kufanikisha jambo hili. Awamu iliyotangulia ya mradi wa uhifadhi wa Kisiwa cha Misali ilimalizika huko Pemba mnamo mwezi November kwa mwaka huo kwa kutoa nafasi ya mradi wa Elimu ya Mazingira kwa maadili ya Kiislamu, kuingia. Ni katika kipindi hicho hicho, ilifanyika warsha iliyojadili njia mbali mbali za kufundishia somo la maadili ya mazingira na Uislamu pamoja na uhamasishaji wake. Kulingana na ushiriki na michango mbali mbali iliyotoka kwa wadau na washiriki kiujumla, warsha ilmalizika kwa kuonyesha mafanikio makubwa. Hii iliwezesha kutoa mwanga kwa mradi wa aina hii kukubalika sio tu na jamii bali vile vile na wadau wengine wa mradi huo.

Katika kongamano la kimataifa lililoandaliwa na shirika la WWF kwa kushirikiana na taasisi za kidini na mambo ya Uhifadhi wa mazingira, ambalo lililofanyika mjini Kathmandu Nepal mnamo mwezi November mwaka 2000, mradi huu ulikuwa ni wa aina yake na wa kipekee kutoka

Afrika kutambuliwa na Jumuiya ya kimataifa kuwa unaoendana na maadili ya jamii husika.

Kiasili, Dini ya kiislamu imeshikamana na imani ya kuyajali mazingira, na tunaweza tukapata jibu sahihi na la kupendezesha tutakapojibu swali namna gani mahusiano ya kiasili baina ya binadamu na viumbe vyengine yalivyopotea. Swali hili halilengi kwa waumini wa dini ya kiislamu tu, bali hata watu wa itikadi nyengine. Hata hivyo hatutaenda kwa undani zaidi kulizungumzia jambo hili katika nukta hii hivi sasa kwani tutaweza kulisoma zaidi katika kurasa zinazofuatia. Kuongezeka mwamko kuhusiana na wasiwasi uliopo baina ya ukuaji wa uchumi na shughuli za uhifadhi wa mazingira kumepelekea majadiliano makubwa ya kimataifa kuelekea mfumo wa maendeleo endelevu ya ulimwengu huu.

Mwongozo huu, ni sehemu ya utekelezaji wa Mradi wa Elimu ya mazingira wa Kisiwa cha Misali – Zanzibar, ambapo awamu ya pili ulianza kwa Warsha iliyowezeshwa na Taasisi ya MacArthur mnamo mwezi January 2001. Mwongozo huu si kitu kipya hasa kwa vile umetegemeza zaidi mafunzo ya Qur'an, lakini kilicho kipya ni kuweka mpangilio wa masomo yake katika mfumo maalum utakaosaidia wenye kukitumia katika maeneo yaliyokusudiwa kufanikisha azma iliyokusudiwa. Uandaaji wa muongozo huu, ni sehemu tu ya juhudi zinazofanyika katika kukumbushia itikadi yetu amabayo wengi wanaona kuwa sio sehemu ya Uislamu. Kiasili, jambo hili halikugawanywa bali lilijumuishwa ndani ya mfumo kamili wa maisha ya mwanadamu. Kilichofanyika hapa, ni kupanda mbegu ya elimu ambazo watu watavuna kutokana na wingi wa mbegu hizo.

"Kiwango kilichofikia mradi huu si kipimo kidogo" maneno haya yalizungumzwa na Bibi Polly Dolan Mratibu wa CARE Tanzania-Zanzibar aliyekuja baada ya kuondoka Bw. Rob Wild, na matarajio yake yalikuwa kuona matokeo mazuri, namshukuru kwa maeno yake hayo na kwa msaada wake aliotupa hapo mwanzoni. Vile vile napenda kuainisha shukrani zangu za dhati kwa wafuatao; Bibi Helen de Jode kwa msaada wake katika hatua mbali mbali za utekelezaji wa mradi huu, wafanyakazi wa Wizara ya Kilimo, Maliasili na mazingira pamoja na iliyokuwa Kamisheni ya Maliasili-Zanzibar, hasa Bw. Thabit Masoud na Rashid Juma, Mufti wa`Zanzibar

na wafanyakazi wake. Napenda kuongezea shukrani zangu za dhati kwa Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mazingira na Ushirika ambapo kwa msaada wake mkubwa umepelekea mafanikio ya mradi huu.

Mwishoni na kwa kiasi kikubwa shukrani zangu za dhati kwa mtayarishaji mwenzangu na mshirika wangu mkuu Bw. Ali Kh. Thani, kwa juhudi na msaada wake usio na kikomo ambao umefanya mwongozo na mradi huu kuwa ni changamoto na uzoefu na somo la aina yake.

Fazlun Khalid
Islamic Foundation for Ecology and Environmental Sciences
Birmingham, England
January 2008

# UTANGULIZI

## Kisiwa cha Misali na umuhimu wake

Sehemu iliyo kubwa ya sayari hii imefunikwa na maji ambapo robo mbili ni maji ya bahari yanayosaidia maisha ya maelfu ya viumbe waliopo ulimwenguni. Tukiachilia mbali, kendelea kupungua kwa wingi maliasili za bahari hususan katika maeneo yenye miamba ya matumbawe na maeneo ya ndani ya uvuvi. Watu wa Pemba, wanakabiliwa na hali ya upungufu wa maliasili muhimu zinazoendelea kutoweka kila leo na kutishia maisha yao. Upungufu huu, unatokana na kuendelea kwa shughuli zisizo endelevu za kibinadamu katika raslimali za pekee za pwani na baharini.

Kiswa cha Misali ni mfano mzuri wenye maajabu ya kimaumbile yaliyo baharini ambapo kutokana na mifumo mbali mbali iliyomo kama vile miamba mirefu ya matumbawe yenye aina tofauti, utando wa majani ya bahari, miti ya mikoko, makome pamoja na aina nyingi za samaki na viumbe vyenginevyo vinavyoishi katika uasili wake ndani ya ulimwengu huu. Miamba ya matumbawe ambayo inakizunguuka kisiwa cha Misali, inawezesha maisha ya aina zisizopungua 300 za samaki na vile vile aina kuu (genera) zisizopungua 42 za matumbawe. Sehemu hizi ni miongoni mwa vivutio vya daraja ya juu kabisa ulimwenguni kwenye fani ya uzamiaji na kuogelea. Wingi wa samaki waliopo katika maeneo hayo, unasaidia maisha ya zaidi wavuvi 1000 pamoja na familia zao ikiwa ni sawa na zaidi ya watu 12,000 wanaoishi kuzunguuka kisiwa cha Pemba.

Ni katika miaka ya karibuni, kuongezeka kwa matumizi ya zana zisizo halali na uvuvi wa kupindukia, kumeripotiwa kusababisha madhara kwa mazingira yaliopo na kupelekea upungufu mkubwa wa samaki. Haya ni matukio ambayo hayakutarajiwa katika historia ya kisiwa hiki, na ikiwa hayatashughulikiwa ipasavyo na kwa haraka, basi ile hadhi ya maeneo ya kisiwa hicho ya kusaidia uendelevu wa maisha ya jamii ya wavuvi wa Pemba inaweza kupotea. Hivyo vizazi viliopo na vijavyo vitakosa kunufaika na wingi wa raslimali hii ya pekee.

## Mradi wa uelimishaji wa maadili kiislamu na mazingira – Misali (Misali Ethics)

Fikra au dhana ya maadili ya Kiislamu kuwa ni sehemu ya uhamasihaji katika kusaidia kuboresha uhifadhi wa kisiwa cha Misali ulitokana na mtizamo wa kijamii na kiutamaduni wa watu wa Pemba ambapo jamii kubwa inayoishi ni waislamu. Hii tunaweza kusema kwa kiasi fulani ni kwa mara ya kwanza mradi wa Utunzaji mazingira yanayozingatia maadili ya kiislamu yamefanikiwa kutumika katika kuhamasisha uhifadhi wa mazingira ya bahari, ambao jamii yenyewe ilihusika kwa kiasi kikubwa kuyaendesha. Hata jamii hii kama zilivyo jamii za sehemu nyingine ulimwenguni, zinakabiliwa na tishio linalosababishwa na harakati za kimaendeleo. Ikiwa jambo hili halitaangaliwa na kushughulikiwa kwa makini litaweza kusababisha uharibifu zaidi wa mifumo ya kiekologia huku muda wa kuweza kurekebisha hali hii ukiwa unapita.

Mradi wa elimu ya mazingira wa Misali, ulishirikisha jamii ikiwemo wavuvi katika maeneo ya yaliyolengwa ndani ya kisiwa cha Pemba. Madhumuni ya mradi huo yalikuwa ni kukuza ufahamu wa jamii kuhusiana na uhifadhi wa maliasli za uvuvi na baadae kuoanisha matokeo na vijiji vyengine ambapo uhamasishaji ulifanyika pasina kuhusisha maadili ya kiislamu. Tukiachilia mbali matumizi ya kitabu hiki, vile vile njia mbali mbali zilitumika ikiwemo; uoneshaji wa video, khotuba za ijumma, mawaidha, mabango pamoja na mashindano ya mashule yaliyondaliwa na kutumika kuhamasisha jamii.

## Uislam na Uhifadhi

### Kuamrishana mema

Msingi uliopo kwenye mahusiano na mawasiliano kwenye dini ya Uislamu ni kufanya matendo mema na kukatazana mabaya. Hili ni jambo la lazima “fardh” na limejengeka kwenye kanuni ya *Amr bil maa’ruf (amrisha mema)*. Kuwaelimisha wengine kuhusiana na maumbile na uasili wa ulimwengu na namna ya kuchukua tahadhari au kuutumikia ni sehemu muhimu katika jukumu hilo. Kitabu hiki kimeandaliwa ili kumsaidia mwalimu

namna ya kuwasilisha ujumbe kwa wengine na kujenga tabia ya kujali mazingira ya bahari.

وَلۡتَكُن مِّنكُمۡ أُمَّةٞ يَدۡعُونَ إِلَى ٱلۡخَيۡرِ وَيَأۡمُرُونَ بِٱلۡمَعۡرُوفِ
وَيَنۡهَوۡنَ عَنِ ٱلۡمُنكَرِۚ وَأُوْلَٰٓئِكَ هُمُ ٱلۡمُفۡلِحُونَ

**“Na wawepo watu miongoni mwenu watakaolingania kuelekea mambo ya kheri, kuamrishana mema na kukatazana maovu. Hao ndio waliofaulu.”**

Al Qur’an 3:104

*“kutafuta elimu ni jambo la lazima kwa kila Muisilamu mwanamume na mwanamke”*

*Sahihi Muslim*

Uhifadhi ni utunzaji ni kuweka kitu chenye umuhimu fulani katika hali ya uangalizi iliyo nzuri ili kisiweze kuharibika. Kwa kuangalia maana hiyo, ikiwa ipo raslimali yenye thamani au mahitaji ya kipekee ambayo na wakati huo huo yanaonekana kuwepo katika tishio la kuharibiwa, basi itahitaji kuwekewa uangalifu maalum wa utunzaji.

Kwa maana nyengine Uhifadhi inatafsiriwa kuwa ni tendo zuri la kulinda au kutunza mazingira asilia yanayotuzunguuka kwa ajili ya manufaa ya wote. Uhifadhi wa mazingira kama inavyofahamika hivi sasa, kwa kiasi fulani ni dhana mpya iliyoibuka karibu miaka khamsini iliyopita kutokana na tahadhari ya matokeo ya shughuli za kibinadamu. Hivi sasa huu umekuwa ni mwelekeo wa ulimwengu katika nyakati hizi. Yote haya yametokea kutokana na hali ya mabadiliko ya tabia za mwanadamu katika kutishia mizan au kutoangalia uwiano uliopo katika kuzingatia vipimo sahihi vya maumbile. Sababu mbili kuu za jambo hilo, ni kukua kwa kasi kwa shughuli za kiuchumi ulimwenguni ambao unaangalia raslimali za dunia kama kitu cha kutumika tu. Hii inaenda sambamba na ongezeko la idadi ya watu ulimwenguni. Katika ripoti iliyotototolewa na shirika la kimataifa la mazingira ulimwenguni (United Nations Environment Programme) inayoitwa “GEO

2000" imejaribu kueleza athari za mazingira zinazosababishwa na binadamu kwa kufafanua kuwa wananadamu wanaendelea kuwa viumbe waharibifu na wavamizi wa raslimali za dunia bila kujali kipimo gani cha matumizi kinahitajika. Ripoti hiyo vile vile inazungumzia namna hali hii inavyoenda sambamba na ongezeko la idadi ya watu kuwa kuwa inatishia kumaliza raslimali ambazo maisha ya watu yanazitegemea.
Ripoti hiyo inaonya kuwa kuwa tuna wakati mdogo sana kwa ajili ya kupanga mipango mizuri yenye uwiano inayoelekea mifumo endelevu ya raslimali zetu bila kuchelewa. Wakati ambapo harakati za kibinadamu zinazopewa jina la maendeleo zinachukua mkondo wake lakini tayari zinaacha athari za uharibifu ambazo zinatishia uhai na maisha ya viumbe wote.

Ingawaje kwa upande wetu haitarajiwi kutokea haya, lakini Zanzíbar kwenye mwambao wa kisiwa cha Misali huko Pemba, kunanyemelea kuingia katika mchakato kama huo. Upande mwengine unaohiotajia kuzingatiwa zaidi pale yanapochukuliwa maeneo ya kisiwa cha Misali kuwa ni kivutio cha kiutalii. Kwa watu wa Pemba na Zanzíbar kiujumla, ni muhimu kutoa jawabu kwa ulimwengu unaoelekeza hivi sasa kuhusiana na mfumo endelevu wa utunzajia wa raslimali. kwa kuzingatia hali halisi ilivyo kwenye kisiwa cha Misali.Kisiwa hiki hivi sasa kinatambulika ulimwenguni kuwa tunzo yenye mazingatio maalum na sehemu ya muhimu ya kuangaliwa kwa kuzingatia namna gani maadili ya kijamii yataweza kusaidia usimamizi endelevu wa raslimali. Hay vile vile yaliaianishwa kupitia kongamano la kimataifa lililojumuisha dini na imani mbali mbali lililofanyika huko Kathmandu, Nepal mnamo mwaka 2000. Hivyo hii ni moja katika hatua muhimu sana na hii ni dalili za kutia moyo katika mwelekeo huu wa kimazingira kimataifa.

Mahusiano yaliopo baina ya maadili ya mazingira na dini ya kiislamu ni kitu kikongwe sana katika mwenendo wa kibinadamu.Tukiangalia historia ya Uislamu, tokea hapo awali, maisha hayakutofautishwa kabisa na baki ya mpangilio asilia wa kimaumbile. Hili linastahiki kuwa ni jambo la kuzingatiwa kila wakati kama vile kila tone la pumzi au hewa tunayoivuta katika mapafu yetu. Kama Allah taala anavytuelezea-

وَلَقَدْ جِئْنَاهُم بِكِتَابٍ فَصَّلْنَاهُ عَلَىٰ عِلْمٍ هُدًى

وَرَحْمَةً لِّقَوْمٍ يُؤْمِنُونَ

Tumewaletea kitabu kinachobainisha kila kitu kwa yakini na uongozi na rehema kwa watu wenye kuamini.
7:52

Sio kwamba Qur'an haikuzungumzia mazingira au masuala ya uhifadhi moja kwa moja kiasi ya kufahamika hii leo. Lakini Qur'an imetumia lugha tofauti kufafanua mambo haya. Lugha ya fitra (hali ya maumbuile asilia aliyoyaumba Allah) imetumika ili kushughulikia mambo hayo. Wanadamu wamekuwa wakiendelea kusishi katika fitra pamoja na kutumikia tabia waliyoizowea wao wenyewe kwa mamia au maelfu ya miaka; ambayo ni kuishi katika hali ya umoja na mazingira yanayowazunguuka. Lakini utamaduni huu, umeachiliwa mbali hivi sasa na kuanza kufata utaratibu mwengine wa maisha usiojali mshikamano wa viumbe

Dini ya Kislamu ni mfumo kamili wa maisha, mbali imani ya kiroho, imejumuisha vile vile mafundisho ya kimila, utamaduni, sayansi, mazingira pamoja na masuala mengine ya kiuchumi na kijamii ambayo kila mmoja wetu anahitajika kuyafahamu ili aweze kutekeleza vizuri dini yake na kuishi ulimwenguni kama anavyohitajika na Mola wake . Suala la utafutaji elimu kwa kila mtu na kwa rika zote ni jambo la wajibu na limetiliwa mkazo sana hasa kwa kuwa ni sehemu kuu ya ibada.

Uhifadhi wa mazingira katika Uislamu ni namna ambavyo mwanadamu anavyotimiza na kuthamini ubinadamu wake. Qur'an inajaribu kufafanua mahusiano hayo ambayo sio kuwa yapo kwetu wanadamu tu, bali vile vile na kwa baki ya viumbe vingine vya ulimwengu huu ambavyo Mola Subhana huu wa Taala ameviumba. Huu ni mtihani kwetu na tunahitajika kuutekeleza ili tupate mafanikio kwa maisha ya sasa na baadae.

لِيَبۡلُوَكُمۡ أَيُّكُمۡ أَحۡسَنُ عَمَلٗاۗ

……ili akufanyieni mtihani yupi kati yenu ni
mwenye matendo mazuri.
11:7

Hivi sasa tuko katika vita vya mazingira yetu yanayotuzunguuka na inaonekana tunakosa kufaulu mtihani tuliopewa na aliyetuumba.

Kile ambacho Mwenyezimungu amekiumba kinachukuliwa kuwa ni alama au ishara za uweza wake. Kwa vile Qur’an ni uthibitisho wa Allah Taala kuwa kila kilichomo ulimwenguni ni milki yake. Aya zifuatazo zinatutaka kuona kuwa ulimwengu wote na kila kilichomo ni alama za kuwep kwake. Misali ni ni dalili zake za uwez wa kuumba na rehma zake kwetu. –

وَفِي ٱلۡأَرۡضِ ءَايَٰتٞ لِّلۡمُوقِنِينَ
وَفِيٓ أَنفُسِكُمۡۚ أَفَلَا تُبۡصِرُونَ

Na katika ardhi zipo dalili kwa watu wenye kutumia akili, na katika nafsi zenu
basi jee hamuonii?
51:20-21

**Mwelekeo**

Allah Ta’ala amesema katika Qur’an “jua na mwezi vyote vinakwenda kufuata njia sahihi iliyowekewa (55:5), ikimaanisha kufata maelekezo maalum. Na hii ni hakika kabisa kwa ulimwengu wote na maumbile yaliyomo ndani yake. Maumbile yote aliyoyaumba Allah Subhana Huu wa Taala yanafanya kazi kwa sababu yamewekewa viwango na taratibu zake za kufanya hivyo. Viwango au mipaka kama hiyo amewekewa mwanadamu

na Qur'an imetaja viwango hivyo kwetu. Hatimaye, *Sheria* ya Kiislamu ambayo imewekwa kwa ajili ya kutuongoza imefafanua mipaka hii. Kuishi bila ya kuvuka mipaka au viwango hivi ni kutii sheria hizi ni katika kutafuta amani inayotakiwa. Hii inafafanuliwa kuwa ni kuishi katika utaratibu halisi wa kimaumbile kutokana na kuvipa haki zake kila kiumbe cha ulimwengu huu kwa mujibu wa sheria.

Kuishi pamoja na viumbe vyengine ndani ya ulimwengu huu, inachukuliwa ni hali ya makubaliano kimaisha, ambapo katika uislamu hakuna kubagua baina ya viumbe alivyoviumba Mwenyezimungu na baki ya viumbe vyengine.

Tatizo liliopo hivi sasa ni kuwa, waislamu wengi tunaishi mbali sana na mafundisho ya sheria na kwa maana hiyo tumepoteza ufahamu wetu unaomhusisha mwandamu na maumbile yake.Tumepotelea mbali mno na katika hali hiyo ni lazima tuangalie mbele kutambua mambo ambayo Uislamu unatuelekeza namna ya kurekebisha tabia zetu kulingana na mazingira tunayoishi . Ikiwa Sheria imefafanuliwa kama ni tandiko lililo pana kabisa ambalo limekusanya mfungamano wa mambo na vitu tofauti, hivyo tunachokifanya hapa ni kuchukua baadhi tu ya sehemu za mkusanyiko wa muunganiko uliopo katika tandiko hilo, na kujaribu kuzituma akili zetu kwa kuzingatia na kuleta maana ya yale yanayohitajika kwa kufata vigezo vya kisheria. Mfumo kama huu unawakilisha mbegu yenye kutoa vioto tofauti vya matunda. Mbegu hii ni *Ilm ul AKh'aalq* (Elimu ya Maumbile) ambayo ni mafundisho ya mazingira katika dini ya Kiislamu. Haya ni mafundisho muhimu na kile ambacho tumekusudia kukifanya katika kurasa zitakazofuatia, ni kutupa utangulizi wa somo hili ambapo Insha Allah (akipenda Mwenyezimungu) litazidi kuboreshwa na wale watakaoshiriki kuutumia muongozo huu.

Masomo sita ya Muongozo huu, kila mmoja ni kiwakalisho cha mfumo mzima wa matunda katika shamba la mbegu na misingi yake inatokana na Qur'an. Tunaweza kuvuna kutokana na hayo kutokana na namna ile tutakayokusudia.

## MATUMIZI YA MWONGOZO HUU

### Makusudio

Muhtasari huu, unalenga juu ya mafundisho ya Qur'an kwa kuhusisha elimu ya mazingira, umetayarishwa ili kuweza kusaidia wanamazingira wakiwemo walimu wa maskuli, jamii kiujumla na watu wengine katika kazi ya upelekaji ujumbe wa uhifadhi wa mazingira kupitia maadili ya kiislamu

Watumiaji wengine ni pamoja na wahadhiri wa vikundi vya kufikisha ujumbe, makhatibu katika swala za Ijumaa na watu wanaotayarisha vielelezo vya kufundishia kwa ajili ya programu za elimu ya mazingira (kama vile mabango, vipeperushi, filamu, matumizi ya radio pamoja na programu za televisheni) pindi watapopendezewa kuhusisha maadili ya kiislamu kuhamasisha utunzaji wa mazingira.

### Masomo yaliyomo

Muongozo huu umejumuisha masomo au sehemu sita ambapo kila mojawapo unatoa ujumbe muhimu pamoja na nukuu ya aya za Qur'ani zinazhusiana na somo lenyewe. Masomo haya yamefuata mpangilio na mtiririko maalum ambapo umeanza na somo la Tawheed (yaani imani ya kumtambua Mwenyezimungu, upweke wake na uweza wake) ambao umegusia mjadala wa ufahamu wa uumbaji wake -Mwenyezimungu Subhana huu wa Taala ambae ndie aliyetuwekea sheria, Tumeweka mjadala unaohusu ufahamu wa maumbile ambayo Mwenyewe ameyaumba, makusudio ya kuwepo kwetu, mwelekeo wa tabia yetu ya kuharibu mazingira na kumalizia na majukumu ambayo tumerithi katika kuchukua dhamana ya ukhalifa. Sehemu au masomo haya yamepangika katika mtiririko wa sura ya kwanza hadi ya sita kama zitakavyoonekana katika kurasa zinazofuatia.

<u>Sura ya kwanza – *Tawhid:*</u> Kuelewa msingi wa upekee/upweke au Umoja wa Muumba yaani Mwenyezimungu, asili ya maumbile, maumbile aliyoyaumba, pamoja na umuhimu wa kuhifadhi maumbile hayo.

Sura ya Pili – *Khalq* (Maumbile): Kufahamu jinsi au vipi Qur'an inazungumzia vitu vinavyohusiana na mazingira na uhifadhi kupitia aya zinazohusiana na uumbaji - Khalq.

Somo la tatu – *Mizan:* Kufahamu msingi wa kipimo sahihi na namna gani ulimwengu unahitajika kuwekwa katika hali nzuri kuelekea uhifadhi wa mazingira na manufaa kwa viumbe

Somo la nne – *Insan* (Kujifahamu Mwanadamu): Kujua ni kwa nini Allah Ta'ala amemuumba mwanadamu na vile vile kujua nafasi zetu katika maumbile ambayo Mwenyezimungu ameyaumba yaani "fitra".

Somo la Tano – *Fasad* (Uharibifu): Kufahamu uwezo wa mwanadamu na tabia zake za uharibifu ambazo zinapelekea athari za kimazingira

Somo la sita - *Khalifa:* Kufahamu majukumu yetu katika ulinzi na Kusimamia Ulimwengu, ikiwemo namna tunavyovichukulia au kuishi na viumbe wengine.

**Muundo**

Ufafanuzi wa kila sura ndani ya muongozo huu unafuata utaratibu wa muundo ufuatao –

| | |
|---|---|
| **UJUMBE** | Unafafanua hali au ujumbe unaowasilishwa. |
| **MADHUMUNI** | Unafafanua kusudio la ujumbe unaoweza kuwa ni mazingitio katika kupeleka ujumbe. |
| **AYA ZA MSINGI KUTOKA KWEYYE** | Nukuu halisi kutka kwenye Qur'an ambazo zinazoelekeza kuhusu ujumbe uliokusudiwa. |

| | |
|---|---|
| **NUKUU ZA ZIADA** | Baadhi ya aya za ziada ndani ya Qur'an ambazo zinatoa ufafanuzi zaidi kuhusiana na ujumbe. |
| **MAJADALA WA ZIADA** | Maelezo ya kundeleza mjadala kwa ajili ya kuendelezea ufafanuzi. |
| **MAHUSIANO NA MAZINGIRA YA BAHARI** | Unatoa utangulizi wa ujumbe unaokusudiwa na namna unavyohusishwa na mazingira ya bahari. |
| **MUHTASARI** | Unatoa muhtasari ya mjadala wa vipengele vilivyovjadiliwa kwenye ufafnuzi unaoendelea. |

Mazingatio: kwa vile kitabu hikli ni kwa ajili ya Muongozo, watumiaji wote wa muongozo huu, wanaombwa kuwa huru kuamua kwa kiasi gani, namna gani na pahali gani wanaweza kutumia kitini hiki baada ya kuyajua mazingira kiujumla.

Wanahimizwa wao wenyewe kuandaa namna watakvyowasilisha masomo kwa kuongeza aya za ziada kutoka kwenye Qur'an na hadithi za mtume S.A.W kulingana na masomo haya sita au zaidi.Wawasilishaji vile vile wanatakiwa kutumia uzoefu wao na kutoa fikra tofauti katika kuendeleza masuala haya.

Walimu wa Madrasa wanaweza kutafuta njia zitakazoweza kuendana na mada au masomo haya pamoja na kujenga ufahamu wa walengwa kulingana na hali iliyopo. Ikiwa mradi utatumia kufanya mashindano baina ya madrasa, wanafunzi wanaweza kuelekezwa namna ya kuandaa tungo au maigizo yatakayotoa mguso wa utunzaji wa mazingira ya bahari kulingana na mafundisho ya kiisalmu. Ni vyema kuandaa muhtasari wa maelezo ya mungozo huu kwa ajili ya wanafunz.

# SOMO LA KWANZA – TAWHID

## UJUMBE

*Tawhid* ni msingi wa dini ya kiislamu ambao unafundisha upekee au Umoja wa Allah Subhana hu Wataala ambae ni Muumba wa kila kitu. Somo hili linatuongoza katika kuanza mjadala kwenye utambuzi wa maumbile yake Allah yaani (khalq) pamoja na umuhimu wa kuyatunza.

## MADHUMUNI

Katika sehemu hii tutaangalia vipengele maalum vya Tawhed ambavyo vitatujenga taswira na hisia juu ya mahusiano yetu na mazingira ambayo ni maumbile kamili aliyoyaumba Allah Taala.

## AYA ZA MSINGI KWENYE QUR'AN

بِسْمِ ٱللَّهِ ٱلرَّحْمَٰنِ ٱلرَّحِيمِ

قُلْ هُوَ ٱللَّهُ أَحَدٌ ﴿١﴾ ٱللَّهُ ٱلصَّمَدُ ﴿٢﴾ لَمْ يَلِدْ

وَلَمْ يُولَدْ ﴿٣﴾ وَلَمْ يَكُن لَّهُۥ كُفُوًا أَحَدٌۢ ﴿٤﴾

Kwa jina la Allah mwingi wa rehema na mwenye kurehemu
Sema: Yeye Mwenyezimungu Mmoja (tu),
Mwenyezimungu (Allah) ndie Anaestahiki Kukusudiwa (na viumbe vyake vyote kwa kuabudiwa na kumuomba na kumtegemea) na yeye ni wa Milele Asiye na Mwisho Hakuzaa wala Hakuzaliwa
Na wala hana anaefanana nae hata mmoja'
112:1-4

Kumjua muumba ni hatua ya mwanzoni katika kufahamu maumbile yake aliyoyaumba na katika sura maarufu sana ndani ya Qur'an - *Sura Al-Ikhlas* (sura ya utakasifu), ambayo husomwa mara kwa mara katika swala zetu imeweka misingi thabiti ya ufahamu.. Hii ni kauli ya uthibitisho wa Upekee (*Ahad*) wa muumba na umoja au upekee au mshikamano wa maumbile yote ambayo mwanadamu ni sehemu ya hayo. Jambo ambalo linazungumziwa sana leo hii ikiwa kama ni njia ya mshikamano kuelekea utunzaji wa mazingira limetokana kimsingi ndani ya maana ya *Tawhid.* Katika aya ya pili Mwenyezimungu Mtukufu anajielezea yeye mwenyewe kuwa ni - *Samad* - yaani ni mwenye kukusudiwa na viumbe vyote kumuabudu, kumuomba na kumtegemea, yeye ni wa milele na kudumu ikiwa inatukumbushia kuwa atatuendeleza au kutudumisha sisi kupitia kile alichokiumba. *Samad* vile vile inatafsiriwa asie na mwisho au asie na mipaka aliekamilika.

## AYA ZA ZIADA KUTOKA KWENYE QUR'AN

*Tawhid* Imefafanuliwa ndani ya mtizamo wa khalq kupitia aya zifuatazo –

***Al Khaliq* (Muumbaji)**

ذَٰلِكُمُ ٱللَّهُ رَبُّكُمْ خَٰلِقُ كُلِّ شَيْءٍ
لَّآ إِلَٰهَ إِلَّا هُوَ ۖ فَأَنَّىٰ تُؤْفَكُونَ

Yeye huyu ndie Mwenyezimungu, ni Mola wenu,
Muumba wa kila kitu,
Hakuna Mwenyezimungu mwengine (anaestahiki kuabudiwa kwa haki)
isipokuwa yeye tu: Basi wapi mnageuziwa?
40:62

هُوَ ٱللَّهُ ٱلْخَٰلِقُ ٱلْبَارِئُ ٱلْمُصَوِّرُ ۖ

Yeye ndie Mwenyezimungu, Muumbaji, Muanzishaji –Mfanyaji/
mtengenezaji, Mfanyaji sura (za namna kwa namna – tofauti)
59:24

***Al Muhit* (mwenye kuvizunguuka kuvijua vitu vyote)**

وَلِلَّهِ مَا فِي ٱلسَّمَٰوَٰتِ وَمَا فِي ٱلْأَرْضِ ۚ وَكَانَ ٱللَّهُ
بِكُلِّ شَيْءٍ مُّحِيطًا

Na ni milki yake Mwenyezimungu vyote vilivyomo mbinguni
na ardhini. Na Mwenyezimungu ndie alievizunguuka
(kuvijua ndani na nje yake) vitu vyote.
4:126

***Al Badi'* (mwanzilishi)**

أَمَّن يَبْدَؤُا۟ ٱلْخَلْقَ ثُمَّ يُعِيدُهُۥ وَمَن
يَرْزُقُكُم مِّنَ ٱلسَّمَآءِ وَٱلْأَرْضِ ۗ

Au yule alieanzisha viumbe kisha atavirudisha, na anaekuruzukuni
kutoka mbinguni na kwenye ardhi…(sie bora?).
27:64

**Vile vile zinagatia –**
Nae ndie alieumba mbingu na ardhi kwa haki (uthibitifu) - 6:73
Ardhi ni ya Mwenyezimungu atamrithisha amtakae - 7:128

**UFAFANUZI WA ZIADA**

*Tawhid* ni msingi wa dini ya kiislamu. Imegawanyika katika sehemu tatu, ambapo kwa mjadala wetu huu tutaiangalia moja katika hizo nayo

ni *Tawhid ar Rububiyyah*. Hii inatutaka wanadamu kuamini kuwa yupo Muumba (Mwenyezimungu) ambae ni Bwana wa kuumba. (Aina nyengine mbili za Tawhid ni *Tawhid al Uluhiyya* – hakuna anaestahiki kuabudiwa isipokuwa yeye Mwenyezimungu, na *Tawhid al Asma was Sifat* –kuamini majina yaliyojumuisha sifa za Mwenyezimungu ni ya peke yake). Kufahamu misingi mikuu ya *Tawhid* kunatusaidia kutambua upweke wa Mwenyezimungu na maumbile yake aliyoyaumba ni ya kuwa pekee. Msingi mkuu wa Tawhid umo katika shahada (kushuhudia), ikiwa ni moja katika nguzo tano za kiislam ambayo kila muislamu anaikubali na ni ukumbusho mkuu wa imani. Nayo ni "*laa ilaha illal lah*" hakuna Mola anaestahiki kuabudiwa kwa haki isipokuwa yeye Mwenyezimungu (*Mwenye jina la Allah*). Na hii inathibitisha umoja au upekee wa Allah ambapo kila kitu kinafuata njia hiyo. Sehemu ya Pili ya shahada ni *Muhammadur Rasulullah* yaani Muhammad ni Mtume wa Mwenyezimungu ambae tunamfata mwenendo wake.

*Shari'a*, kama tunavyojua zinatokana na Qur'an na sunna za Mtume Muhammad (S.A.W) kama zilivyotafsiriwa kutokana na mafundisho hayo. Kifungu hiki cha ufahamu kina mengi ya kutufahamisha kuhusiana na mahusiano yetu na mazingira yanayotuzunguuka.

Tawheed ni somo pana ambapo *Rububiyyah* inabeba sehemu kubwa ya haya. Hii inatuelekeza katika kazi ya Allah Ta'ala' ambayo kiujumla imejengeka katika *al asma ul husna (majina matukufu ya Allah)* ambapo machache katika hayo yameorodheshwa katika aya tuliyoijadili hapo juu *Al Khaliq* – Muumba, *Al Bari'* – Mwanzilishi, *Al Musawwir* – mtengenezaji sura tofauti, *Al Muhit* – Mwenye kuwazunguuka kuwajua waja wake –kila kitu, *Al Badi'* – Mwanzilishi wa kila kitu. Tukiendelea zaidi, *Rububiya* inatufundisha kuhusu kazi ya uumbaji kuwa ni ya Allah Ta'ala peke yake. Yeye ndie aliesanii na mtengenezaji wa *Al Alamin* (ulimwengu wote) na aya zifuatazo zinaelezea mchakato huo kwa kutumia maneno kama fatara kuviumba au kuvipa uhai (kuvizalisha) na *anzala* (kuteremsha ardhini).

**Fatara (kuumba)** – Neno hili linatokana na msingi wa **F T R** kwa maana nyengine yenye ufafanuzi wa ziada kwa maana ya ufa au mpasuko au mripuko.

إِنِّي وَجَّهْتُ وَجْهِيَ لِلَّذِي فَطَرَ ٱلسَّمَٰوَٰتِ وَٱلْأَرْضَ

Mimi nimeelekeza uso wangu kwa yule alieziumba mbingu na ardhi.
6:79

***Anshaa'* (kuumba/kuitoa/kuizalisha/kuianzisha) –**

وَهُوَ ٱلَّذِيٓ أَنشَأَ جَنَّٰتٍ مَّعْرُوشَٰتٍ وَغَيْرَ مَعْرُوشَٰتٍ
وَٱلنَّخْلَ وَٱلزَّرْعَ مُخْتَلِفًا أُكُلُهُۥ وَٱلزَّيْتُونَ
وَٱلرُّمَّانَ مُتَشَٰبِهًا وَغَيْرَ مُتَشَٰبِهٍ

Naye Mwenyezimungu ndiye aliyeiotesha miti (inayoegemezwa katika chanja katika kuota kwake) na isiyoegemezwa, na (akaotesha) mitende na mimea yenye matunda mbali m,bali, na (akaumba) mizaituni na mikomammnga, inayofanana na isiyofanana.
6:141

***Anzala* (kuteremsha) -**

وَأَنزَلْنَا مِنَ ٱلسَّمَآءِ مَآءً فَأَنۢبَتْنَا فِيهَا
مِن كُلِّ زَوْجٍ كَرِيمٍ

Na tumeteremsha mvua kutoka mawinguni
Na tukaotesha kila aina ya mimea kuota/kukua kwenye ardhi.
31:10

## MAHUSIANO NA MAZINGIRA YA BAHARI

Tukiangalia tena aya zilizopita tutaelewa kwa makini ushahidi madhubuti unaotambulisha mazingira ya baharini kuwa ni kwa ajili yetu.. Allah Ta'ala ameumba kila kitu (40:62): ikiwemo bahari na kila kilichomo ndani yake. Akakipatia kila kimoja maumbile yake (yanayostahiki) (59:24): yaani hali ya maumbile ya miamba ya matumbawe, samaki na viumbe vyenginevyo vinavyoishi ndani yake kwa kuzingatia maumbile ya kuwepo kwake, mkusanyiko wa kikemikali na uasilia uliopo. Yeye (Allah) anakuruzukuni kutoka mbinguni na ardhini. (27:64) na hii inafafanua zaidi neno *As Samad* katika aya ya msingi. Ardhi (*ard*) neno linalojumuisha mazingira yote ya baharini na nchi kavu. Vile vile tamko la kuotesha linahusiana na kila kitu kilichomo ndani ya bahari ikiwemo miamba ya matumbawe na wingi wa samaki. Uoteshaji huo unahakikisha kuendelea na kudumisha maisha ya viumbe.

## MUHTASARI

*Tawhid* ni msingi wa *Din al Islam*. Inathibitisha ufalme wa pekee wa Allah Ta'ala juu ya kila alichokiumba ambapo hiki ni kielelezo cha uwezo wake. Huu ni msingi wa mshikamano ndani ya dini ya kiislamu. Kama ilivyokuwa *Al Muhit* Allah Ta'ala amekijumuisha kisiwa cha Misali katika mkusanyiko wake wa uumbaji na kuendelea kukihuisha ili kuendeleza uhai wetu.

## SOMO LA PILI – KHALQ

### UJUMBE

*Khalq* ni neno linalotumika katika Qur'an kufahamisha maumbile ambayo Mwenyezimungu ameyaumba. Ni neno linalojumuisha kila kitu tunachokiona ambacho kinatuzunguuka tukiwemo sisi wanadamu. Neno Mazingira laweza kutumika kuwa ni mbadala wa Khalq katika hali na mara nyingi sana

### MADHUMUNI

Katika sehemu hii, tunajadili Khalq tunaanza kuangalia namna gani Din al Islam inashughulikia mazingira na mambo yanayohusiana na utunzaji wake.

وَخَلَقَ كُلَّ شَيْءٍ فَقَدَّرَهُ تَقْدِيرًا

…na (Allah) ameumba kila kitu na akakikadiria kipimo chake.
25:2

Aya hii inatupa maana rahisi na ya moja kwa moja ya mazingira. Msingi wa neno hapa ni *khalaqa* (ameumba). Mwenyezimungu ameumba kila kitu katika dunia hii ikiwemo jamii ya wandamu. Zaidi ya hayo upo ule uhalisi/ukamilifu wa maumbile ambayo inatuonesha vitu viwili. Kimojawapo ni majukumu yaliyopo mbele yetu ya kufahamu na kutengeneza au kuulinda uhalisi/ukamilifu huu. (Angalia somo la sita *Khalifa*). Nalo ni kutunza au kuhifadhi na jengine ni kuangalia vipimo au kiasi.

Maneno yanayotokana katika msingi wa lugha ya kiarabu Q D R ambalo limejitokeza mara mbili katika aya hii. Maneno haya ni kama *qaddara* (kukadiriwa, kuumbwa, kuamrishwa) na *taqdir* (kipimo, uhakika au ukamilifu) na maneno kama kupima, kanuni, kuwa na uwezo au nguvu, pamoja na maneno mengineyo yanajumuisha kundi la maneno yaliyoazimwa kutokana na chimbuko hilo. Hii inatupelekea sisi kuuliza maswali

kuhusiana na kipimo chenyewe. Kwa vile maulizo ya kisayansi, ambayo siyo tu yanayotufahamisha kuhusiana na maumbile asilia ya ulimwengu kama yalivyo au yatakavyokuwa, lakini vile vile yanatufahamisha sisi juu ya uharibifu na uchafuzi tunaosababibisha ndani ya dunia. (Angalia vile vile somo hili katika Mizan na *fasad*)

## AYA ZA ZIADA KUTOKA KWENYE QUR'AN

Neno *khalq* linatokana na msingi wa neno la kiarabu KH L Q na inakadirwa kuwepo aya zisizopungua 261 katika Qur'an ambazo zipo katika mpangilio tofauti wa kilugha (kinahau) ndani ya msingi huo. Aya hizi zimejumuisha marejeo mbali mbali kwa ulimwengu wa kibinadamu, wanyama, misitu, bahari, jua, mwezi na nyota. Aya ya mwanzo ya Qur'an iliyomteremkia Mtume Muhammad (SAW) imelitumia neno hili katika hali yake ya kitendo au amri ili kuweza kuleta athari inayokusudiwa.

اقْرَأْ بِاسْمِ رَبِّكَ الَّذِي خَلَقَ
خَلَقَ الْإِنسَانَ مِنْ عَلَقٍ

Soma kwa jina la Mola wako Aliyeumba.
Amemuumba mwanadamu kwa pande la damu
96: 1-2

Aya zifuatazo zilizochaguliwa kutokana na kiini cha neno Kh L Q zinaonesha uzito na upeo wa jambo hilo lilivyoelezwa katika Qur'an

**Jua, Mwezi...**

هُوَ الَّذِي جَعَلَ الشَّمْسَ ضِيَاءً
وَالْقَمَرَ نُورًا وَقَدَّرَهُ مَنَازِلَ لِتَعْلَمُوا عَدَدَ السِّنِينَ

وَٱلْحِسَابَ ۚ مَا خَلَقَ ٱللَّهُ ذَٰلِكَ إِلَّا بِٱلْحَقِّ ۚ
يُفَصِّلُ ٱلْءَايَٰتِ لِقَوْمٍ يَعْلَمُونَ

Yeye Mwenyezimungu ndiye aliyelifanya jua kuwa mwanga na mwezi kuwa nuru na akaupimia vituo (huo Mwezi) ili mjue idadi ya miaka na hesabu nyenginezo. MwenyeziMungu hakuviumba vitu hivyo ila kwa haki (makusudio maalum). Anapambanua aya zake kwa watu wanaotaka kujua.
10:5

**Mbingu na Ardhi …**

إِنَّ فِى ٱخْتِلَٰفِ ٱلَّيْلِ وَٱلنَّهَارِ
وَمَا خَلَقَ فِى ٱلسَّمَٰوَٰتِ وَٱلْأَرْضِ
لَءَايَٰتٍ لِّقَوْمٍ يَتَّقُونَ

Hakika katika mfuatano (wa daima) usiku na mchana.
Na katika alivyoviumba Mwenyezimungu katika mbingu na ardhi; ziko dalili (za dhahiri za uweza wake Mwenyezimungu) kwa wanaomuogopa Mwenyezimungu.
10:6

**Wanyama …**

وَٱلْأَنْعَٰمَ خَلَقَهَا ۗ لَكُمْ فِيهَا دِفْءٌ
وَمَنَٰفِعُ وَمِنْهَا تَأْكُلُونَ

Na amewaumba wanyama katika hao mnapata vitu vitiavyo joto na manufaa mengine na wengine mnawala.
16:5

**Wanyama kutokana na maji ….**

وَٱللَّهُ خَلَقَ كُلَّ دَآبَّةٍ مِّن مَّآءٍ ۖ فَمِنْهُم مَّن يَمْشِى عَلَىٰ بَطْنِهِۦ وَمِنْهُم مَّن
يَمْشِى عَلَىٰ رِجْلَيْنِ وَمِنْهُم مَّن يَمْشِى عَلَىٰٓ أَرْبَعٍ ۚ يَخْلُقُ ٱللَّهُ مَا يَشَآءُ ۚ
إِنَّ ٱللَّهَ عَلَىٰ كُلِّ شَىْءٍ قَدِيرٌ

Mwenyezimungu ameumba kila kinyama kutokana na maji, baadhi yao wanakwenda kwa kutumia matumbo (wanatambaa) wengine wanatumia miguu miwili, wengine minne. Mwenyezimungu anaumba atakavyo. Mwenyezimungu ni muweza juu ya kila kitu
24:45

**Vile vile zinagatia –**

(Mola wetu) ni yule aliekipa kila kitu umbo lake, kisha akakiongoza (kufuata kinachowafiki umbo lake) - 20:50
Na ambae ameteremsha maji mawinguni kwa kiasi (kipimo maalum)- 43:11
Hatukuziumba mbingu na ardhi wala yaliomo baina yake ila kwa haki na kwa muda uliowekwa…. - 46:3

## MAZINGATIO ZAIDI

Kama aya za msingi zinavyobainisha kwa uwazi kuwa *Khalq* inafafanua kila kitu kuanzia vitu vidogo sana hata visivyoonekana kwa macho hadi vitu vikubwa sana. Wafasiri wa Qur'an kama Ibn Kathir ametafsiri ulimwnegu kama *'alamin* kujumuisha viumbe vyote vinavyoishi katika anga,ardhi na bahari.. Aya ya Mwanzoni katika sura-ti-fatha ndani ya Qur'an inatumia neno hili –

ٱلْحَمْدُ لِلَّهِ رَبِّ ٱلْعَٰلَمِينَ

Shukrani zote zinamthibitikia Allah, Mola wa ullimwengu
(walimwengu) wote.
1:1

Ni muhimu kuwa tunarejea au kukariri ayah ii katika kila rakaa (kipengele) ndani ya swala zetu tano kila siku.

*'Alamin* inaweza kuonekana kujumuisha na kuielezea *khalq* kuingiza vitu ikiwemo vitu vyote vyenye kuonekana ndani ya ulimwengu..vile vile neno *'alamin* linatafsiriwa na wanachuoni wengine kuwa ni Ulimwengu.

Tumeweza kuelezea mahusiano au kiungo kilichopo baina ya dini ya Kiislamu na uhifadhi au utunzaji wa mazingira mwanzoni mwa mwongozo huu na ufuatao ni ufafanuzi zaidi wa haya.

Aya ya utangulizi katika sehemu hii inatukumbushia kuwa Mwenyezimungu Mtukufu ameumba kila kitu. Aya za ziada zinahusisha kuwa jua, mwezi, anga, ardhi na viumbe vyote pamoja na kila aina ya mnyama katika maji. Hii ni tafsiri ya kiujumla ya mazingira na zipo aya nyingi za namna hii. Wakati Mwenyezimungu aliposema kuwa ameumba kila kitu, ina maana halisi kuwa hakuna kilichosahaulika au kuachwa ikiwemo hewa tunayoivuta, maji tunayokunywa na ardhi tunayoitumia.
Ardhi ni sehemu pekee ambayo tunashirikiana kuishi pamoja na mamilioni ya aina za viumbe wengine ambao wengi wao hatujaweza kuwatambua hadi sasa. (16:8). Ardhi inatuwezesha sisi na baki ya viumbe vyote kupata mahitaji yetu. Ni zawadi au neema (n'iima) kutoka kwa Mola wetu kwa kila rika la watu kuanzia waliopita, waliopo na wajao ndani ya ulimwengu huu. Hata hivyo, mwanadamu ni kiumbe wa pekee katika kusababisha uharibifu usiotarajiwa kwenye mfumo mzima wa kiekologia na tishio kwa mfumo wa maisha ambapo viumbe vyote vinautegemea. Ni jambo la kushangaza kuona kuwa, mazingatio yetu katika suala hili la uhifadhi au kutokuwa na matumizi ya busara ni madogo sana na ndiyo yanayobainisha kutofaulu kwetu katika kutekeleza majukumu yetu.

Tutaweza kuona jinsi gani Qur'an inatufunza namna ya kuhifadhi mazingira katika sehumu zitakazofuatia.

## MAHUSIANO NA MAZINGIRA YA BAHARI

Wakati Allah Ta'ala aliposema kwenye Qur'an "Tumeumba "kila kinyama kutokana na maji (24:45), hii imekusudiwa kumaanisha kuwa, sisi kama wanadamu tumeingizwa katika utaratibu huu mzima, halkadhalika maji yanaweza kutafsiriwa wakati mwengine kuwa ni bahari.

Inakadiriwa kuwa, kiasi ya robo mbili ya mwili wa Binadamu umeumbwa kwa maji. Maelezo haya yameelezwa na kunukuliwa katika Qur'an karne nyingi ziliozopita kabla ya ugunduzi wa kisayansi wa hivi sasa. Na vile vile ni sahihi kuwa, sehemu yote ya maisha, wanyama na mimea yenye rangi ya kijani inategemea maji au bahari kupata chanzo chake cha unyevu ambao unatupa uhai.

Bahari, kwa maana hiyo, ina faida kubwa kwetu kwa kutuhudumia uhai wetu wakati huo huo tusisahau namna inavyoatupa uhai kutokana na kubaki katika kina chake cha kawaida. Qur'an inazungumza:

Mmehalalishiwa mawindo ya baharini, na chakula chake - 5:96

Na zipo kwake Mwenyezimungu funguo zote za siri na hakuna azijuaye isipokuwa yeye tu na anayajua yaliyomo baharini na nchi kavu. na haidondoki jani ila analijua. wala haianguki punje katika giza la ardhi (ila anaijua) wala hakianguki - kilichorutubika wala kilichoyabisika (ila anakijua) (hapana chochote) ila kimo katika kitabu kinachodhihirisha Kila jambo - 6:59

Bila ya Misali au maeneo mengine mfano wa hayo duniani, pengine pasingekuwapo Miamba ya matumbawe ambapo kwa mujibu wa wataalamu wa elimu ya miamba, miamba ya aina hii humea au kupatikana zaidi katika maeneo ya bahari yaliyo lingana na maeneo yanayozunguuka kisiwa. Mazingira kama hayo, hayapatikani katika bahari kubwa zenye kina kikubwa.

Miamba ya matumbawe inaweza kufananishwa au kuhusishwa na msitu wa

juu wenye mfumo wake kamili wa kiekologia ambapo miti inatoa kivuli au sehemu ya maisha kwa ajili ya ndege na aina nyengine ya vinyama ili kuweza kukamilisha mfumo mzimo tegemezi wa upatikanaji chakula.Sisi ni wanufaika wakubwa kabisa katika mfumo huu kama ambavyo tunavyonufaika kwa hali ya juu kutokana na mfumo wa upatikanaji wa chakula ambao miamba ya matumbawe unasaidia kutoa tija.kama ilivyo miti au mimea, matumbawe ni viumbe hai vile vile, yanakua au kuhuika na baada ya muda yanakufa au yanaathirika kutokana na namna yanavyotumiwa.

## MUHTASARI

Neno "khalq" limetumika katika Qur'an katika kila dhana inayokubalika kuelezea kile tunachokiona, tunachokihisi, na kupata mguso wake ikiwemo sisi wenyewe. Kuna mamilioni ya viumbe na miti ambayo Allah Ta'ala ameviumba na akaumba mamilioni ya nyota katika anga ambavyo bado kugunduliwa na mwanadamu. 'Alamin imetumika katika aya ya msingi ya Qur'an ikiwa kama kumbukumbu rejea kuelezea vile ambavyo Mwenyezimungu ameviumba.

Neno mazingira ni jumuisho la maana likimaanisha mambo ambayo yanatuzunguuka au mkusanyiko wa maeneo maalum. Tunajua kuwa Kisiwa cha Misali ni maumbile ambayo Mwenyezimungu ameyaumba na tunayahusisha vile vile kama ni eneo lenye mazingira yake ya juu na baharini. Katika maana pana tunaweza kusema kuwa, Misali ni sehemu ya mazingira ya Bahari na inabeba nafasi ya pekee ikiwemo bahari, matumbawe na samaki waliomo katika kutengeneza uwiano muafaka wa kiekologia katika eneo hilo.

Usimamizi wa mazingira ni jambo ambalo limefungamana mno na mwenendo wa dini ya Kiisalm. Jambo hili, bila ya shaka, linaonekana wazi tutapoliangalia ndani ya Qur'ana na Sunna kama tunavyokusudia kufanya hivi sasa.

Ingawaje haichukuliwi kama ni somo pekee. Lakini ni jambo linalotakiwa kuangaliwa kila leo na kuwa ni kielelezo cha kila jambo tulifanyalo.

Uhifadhi ni ufanyaji wa matendo mazuri na kuchunga au kuangalia maisha ya viumbe vyengine (angalia somo la *Khalifa*). Uharibifu wa matumbawe ni tabia mbaya inayopelekea kuangamiza makazi ya viumbe na uwiano murua wa mifumo ya kiekologia. Ni tabia mbaya inayopelekea kunyima fursa kwa wenzetu pamoja na uendelevu wa maisha ya vizazi vijavyo.

# SOMO LA TATU - MIZAN

## UJUMBE

*Mizan* ni dhana ya kuzingatia vizuri kipimo halisi ambacho viumbe vyote vinatumikia na kujiendeleza wenyewe katika uwiano maridhawa. Kutunza au kuhakikisha uwiano mzuri na umarudufu wa mifumo yote miwili ya kiekologia ya baharini na nchi kavu kunasaidia kuhifadhi mazingira.

## MADHUMUNI

Kufikia ufahamu wa *Mizan* na usalama unaohitajika katika kuangalia vitu ambavyo Allah Ta'ala ameviumba.

Katika moja ya sehemu yenye nguvu na maarufu Qur'an al Karim inafafanua maumbile kuwa –

ٱلرَّحۡمَٰنُ عَلَّمَ ٱلۡقُرۡءَانَ خَلَقَ ٱلۡإِنسَٰنَ
عَلَّمَهُ ٱلۡبَيَانَ ٱلشَّمۡسُ وَٱلۡقَمَرُ بِحُسۡبَانٍ
وَٱلنَّجۡمُ وَٱلشَّجَرُ يَسۡجُدَانِ
وَٱلسَّمَآءَ رَفَعَهَا وَوَضَعَ ٱلۡمِيزَانَ
أَلَّا تَطۡغَوۡاْ فِي ٱلۡمِيزَانِ وَأَقِيمُواْ ٱلۡوَزۡنَ
بِٱلۡقِسۡطِ وَلَا تُخۡسِرُواْ ٱلۡمِيزَانَ

Kwa jina la Mwenyezimungu Mwenye kuneemesha neema kubwa kubwa, na Mwenyekuneemesha neema ndogo ndogo.

1 (Mwenyezimungu) Mwingi wa rehema.
2. Amefundisha Kurani.
3.Amemuumba binadamu.
4.Akamfundisha kunena (ubainifu)
5.Jua na mwezi huenda kwa hisabu (yake).
6.Na miti midogo na mikubwa yote inamnyenyekea (Mwenyezimungu).
7.Na mbingu ameziinua juu na ameweka uadilifu.(insafi).
8.Ili msidhulumu katika kupima na (mengineyo).
9.Basi pimeni kipimo kwa haki na wala msipunguze mizani.
55:1-9

Kitangulizi cha aya zilizotajwa kinaanza kwa kutukumbusha maumbile ya pekee kwa kiumbe mwanadamu katika uumbaji. Ufahamu na uwezo wetu wa kuainisha kwa uwazi makusudio yetu kwa uwazi ndio yanayotutofautisha na viumbe vingine vilivyomo duniani.. Mwenyezimumngu Mtukufu ametuzawadia akili (maarifa, ubainifu) ambavyo ni nyenzo kubwa ya kutofautisha kati ya baya na jema, halali na haramu, uaminifu na ukhiana, kuhifadhi na kufisidi, uadilifu na dhulma, matumizi mazuri na mabaya na vile vile kuharibu na kutengeneza.

Imetajwa kuwa Jua, mwezi, nyota ni vitu vyenye mahusiano ya karibu sana na maisha yetu, ikiwa pamoja na miti na mimea vyote vinafanya kazi ya ziada ya kutekeleza utiifu kwa Muumba. Kwa Muislamu anaemuogopa Mwenyezimungu (aya hizi zinafahamisha kwa undani zaidi katika kufahamu hali halisi ya makususdio ya kuumbwa viumbe.

Kila kitu mfano wa mwili wa Mwanadamu, kijaraha kidogo hupona katika muda uliokadiriwa na pasiwe na kovu. Vidonda vingine hupona na kuacha kovu. Banguzi husababisha ulemavu na kuufanya mwili usifanye kazi zake kikawaida.

Hali halisi ni kuwa tunaweza kuangalia ulimwengu unaotuzunguuka na kufahamu kwa njia hii kwa sababu kila kitu kimekusanywa kwa ajili yetu. Kinachoshangaza ni kuwa, sisi wanadamu ni viumbe pekee katika maumbile haya ya ulimwengu ambao kupitia zawadi tuliyoruzukiwa na

Allah ya kufahamu mema na mabaya tuyafanyayo tunachagua kutotii na kuharibu kila kitu kinachotuzunguuka kwa kujiona kuwa ni mahodari.

## AYA ZA ZIADA KWENYE QUR’AN

أَوَلَمْ يَرَوْا إِلَىٰ مَا خَلَقَ ٱللَّهُ مِن شَيْءٍ

يَتَفَيَّؤُا ظِلَٰلُهُۥ عَنِ ٱلْيَمِينِ وَٱلشَّمَآئِلِ سُجَّدًا لِّلَّهِ وَهُمْ دَٰخِرُونَ

وَلِلَّهِ يَسْجُدُ مَا فِي ٱلسَّمَٰوَٰتِ وَمَا فِي ٱلْأَرْضِ مِن دَآبَّةٍ

وَٱلْمَلَٰٓئِكَةُ وَهُمْ لَا يَسْتَكْبِرُونَ

Je! Hawaoni kila vitu alivyoviumba Mwenyezimungu –
ambavyo vivuli vyake vinazunguuka kutoka kulia na kushoto –
vinavyomsujudia yeye , hali ni vyenye kumnyenyekea kiukamilifu?
Na vinamnyenyekea (vinamsujudia) Mwenyezimungu viumbe vyote
vilivyomo mbinguni na ardhini, katika wanyama na malaika pia nao
hawatakabari
16:48-49

**Vile vile zinagatia –**

Na tumeotesha kila kitu kwa kiasi (chake) - 15:19
Na tumekufanyieni humo vitu vya kuendesha maisha yenu….. - 15:20
Wala hatukukiteremsha (chochote) ila kwa kipimo maalum.(si ovyo ovyo tu) - 15:21

## MAZINGATIO YA ZIADA

Moja katika maana tunayoweza kuichukua kwenye neno au tamko *mizan* katika aya za msingi hapo juu ni kule kuamrishwa na Allah Ta’ala kuwa ni sehemu ya maumbile asilia na kushughulikia kwa kuangalia ndani yake juu

ya vipimo sahihi. Ubora wa wa mazingira umeelezewa ndani ya Al Qur'an katika hatua mbili. Kwanza kama tulivyokwisha kuona katika kipengele cha uwiano , ambacho hutegemea kujisalimisha kwa viumbe vyote vilivyobakia katika kutii amri ya muumba. Jambo la pili ni namna ya kuweza kufikia vipimo sahihi kama tulivyojadili katika somo lililopita.

Tamko *Mizan* linatoka katika msingi WZN na tamko *wazan* likimaanisha kupima kipimo. Mizaan inamaanisha uwiano au kipimo na maneno haya mawili yanatumika pamoja katika nyakati nyingi yanapotumika kuelezea uadilifu kuonesha maana yenye nguvu kama ilivyo katika aya

Basi pimeni kipimo kwa haki wala msipunguze - 55:9

Katika sura ya 15:19-21 maneno yaliyopewa taaliki WZN na QDR (angalia sehemu iliyotangulia) zimewekwa pamoja. Allah Taala amefanya kila kitu kinakwenda kwa mizani (*mawzuun* kutokana na msingi WZN) na akateremsha kila kitu katika kipimo kinachojulikana (Qadr kutokana na msingi wa neno QDR). Dhana ya uwiano na kipimo umejitokeza mara nyingi katika Qurani, kutukumbushia juu ya asili ya maumbile.

Inapendezesha kuona kuwa maneno haya yaliyo sawa na yenye nguvu yanatumika kuhusisha matunzo ya mayatima. –

"wala msitumie mali ya mayatima isipokuwa
kwa njia bora… Mpaka afikie balekhe–
Na kamilisheni vipimo vyenu kwa njia ya uadilifu
6:152

## UHUSIANO NA MAZINGIRA YA BAHARI

Ni rahisi kuona uwiano uliopo katika maumbile tukiangalia namna ya miamba ya matumbawe, pepo na dhoruba, tabia ya bahari ya kupungua na kujaa pamoja na mawimbi makubwa. Kisiwa cha Misali ambacho chenyewe kimekuwepo kutokana na miamba ya matumbawe ni sehemu ya mfano wa

uwiano ulio mzuri kwani pindi isingekuwapo Misali pasingekuwepo miamba hiyo ya matumbawe na kwa maana hiyo samaki vile vile wasingekuwapo. Ni muhimu kuangalia jambo hili kwa upeo ili kupata mwanga wa Misali katika mizan ya maumbile aliyoyaumba Allah Ta'ala.

Mifumo yote asilia ya kiekologia iliyopo katika ardhi imejengeka katika maumbile ya uwiano (yaani ipo katika kipimo maalum kinachotegemeana). Mtandao wa mfumo wa upatikanaji wa chakula unajumuisha pande zote za nchi kavu na baharini na unaweza kuathiriwa au kuharibiwa kutokana na mabadiliko ya hali ya kimazingira.. Mabadiliko haya yanaweza kuwa ya kimaumbile au yanayosababishwa na mwanadamu kama ilivyo katika kisiwa cha Misali. Kipimo hiki cha uwiano, au *mizan*, ni kisaidizi kinachoruhusu mfumo wa kiekologia kusaidia maisha ya miti, wanyama na wanadamu (J. Francis…et al…2000).Miamba ya matumbawe,majani bahari, mwani na maeneo ya miti ya mikoko, yanalinda maisha ya samaki wachanga na na mazingira ya bahari kiujumla. Ikiwa tutayaharibu mazingira haya na kuwavua samaki hawa katika hali ya uchanga ndani ya maeneo haya, basi ule uwiano wa mazingira au mfumo wa kiekologia utakuwa umeharibiwa.

Miamba ya matumbawee ni miongoni mwa maumbile yenye kuvutia sana. Yanajumuisha viumbe vya rangi tofauti na ni sehemu yenye kutoa mahitaji muhimu sana kwa mwanadamu. Matumbawe yanasaidia makaazi ya aina kwa aina na maisha ya viumbe tofauti.viumbe hivi vina utofauti katika kuhimili kiwango au ukubwa wa mawimbi, mwangaza, kiwango cha mwani na vyakula vyenginevyo ambapo hukusanyika kufanya kazi ya pamoja (Lieske and Myers 1994). Maisha ya vijinyama vya matumbawe yanahusiana au yanategemeana sana na maisha ya viumbe wa aina nyengine walipo baharini.Uhusiano huu kisayansi unaitwa simbiosis (maisha au uhusiano wa kutegemeana baina ya viumbe vyenye uhai)

Kipo kiungo cha karibu cha namna binadamu wanvyoitumia miamba ya matumbawe na historia za maisha yao.Watu wanahitajika kuweka kipimo kizuri kupitia matumizi endelevu na uhifadhi wa miamba hiyo kwa kutumia njia bora za uvuvi.

Miamba ya matumbawe ni mfumo halisi wa kiekologia wenye wingi wa makazi ya viumbe wa aina tofauti, vile vile sehemu hizi ni moja katika sehemu za baharini zenye kujulikanwa na kutembelewa sana. Wanasayansi wamegundua kuwa, wingi wa aina za viumbe unaokuwepo katika sehemu fulani, hupelekea ufanisi mkubwa wa nyenendo au michakato ya kibaologia katika eneo hilo. Vile vile kwa upande mwengine, inathibitishwa kuwa kuwepo kwa wingi wa aina za viumbe vinavyofanya shughuli zenye kufanana hupelekea kuunda mfumo imara wa kiekologia.

Ikiwa ni sehemu ya mfumo wa kiekologia, miamba ya matumbawe inasaidia kutoa chakula na makazi kwa vijinyama kama samaki, kaa, kamba, na viumbe vyengine vya baharini.Vile vile inafanya kazi muhimu ya kukinga fukwe za pembezoni mwa bahari kutokana na mmon'gonyoko. Hii inatokana na kuwepo kwake kama vizuizi vya kimaumbile dhidi ya mawimbi makali.ya baharí.

Halkadhalika, vile vile ni chanzo cha upatikanaji wa mchanga kutokana na kuvujinkavunjika vipande vidogo vidogo vya matumbawe na kupelekea kupata fukwe na mandahri nzuri pembezoni mwa bahari. Hatimaye hii husaidia kutoa mandhari na vivutio vizuri wa wanadamu ikiwemo vivutio vya kitalii hususan, wazamiaji na waogoleaji. Kwa upande mwengine baadhi ya vijinyama vya matumbawe ni mashuhuri katika utengenezaji wa madawa mbali mbali ambayo hutoa tiba kwa baadhi ya maradhi.

Kwa maana hiyo, ikiwa miamba ya matumbawe itaharibiwa basi uwiano wa maisha na uimarikaji wa mifumo mzima wa kiekologia kwa viumbe vilopo basi utaathirika. Hivyo hivyo, samaki wanaokula pamoja na vijinyama vya matumbawe watabadili tabia ya ulaji au kuanza kutoweka kuelekea sehemu nyengine.

Mfano mwengine ni kuwa, kuvuliwa zaidi kwa samaki wanokula mwani kutasababisha kuongezeka na kukua kwa mwani huo, ambapo husababisha athari mbaya au kuangamiza baadhi ya aina za vijinyama vya matumbawe. Hii ni baadhi ya mifano wa yale yanayofanyika kwenye uharibifu wa kimoja katika mfumo wa kiekologia basi hathiri shughuli za mfumo mzima kutokanana uhusiano uliopoa tangu hapo awali.

Uvuvi wa kuwakusudia aina moja tu ya samaki unaweza kubadili tabia ya uwiano mzuri wa kimazingira kwa vile aina mbali mabli za viumbe vinavyoishi mahali hapo huunda mfumo tegemezi wa upatikanaji cahkula kwa wote. Baadhi ya aina za samaki huwa na tabia ya kula viumbe kama urumba na kiti cha pweza ambao wao hula vijinyama vya matumbawe.Basi ikiwa tutawavua kwa wingi aina za samaki hawa, hivyo idadi ya walaji wa vijinyama vya matumbawe itaongezeka na hatimae matumbawe kuharibiwa kabisa.

Ni sawa kabisa vile vile tunapozungumzia juu ya uvuvi wa kupindukia wa samaki wanaokula mwani hivyo kusababisha ongezeko la mwani huo, vile vile na ongezeko la aina nyingine katika mtandao au silesile ya ulaji au mfumo tegemezi wa upatikanaji wa chakula (Westmacott et al.2000)

Mbinu za uvuvi za kuangamiza kama vile utumiaji wa miripuko au baruti, nyavu za macho madogo(kinia) namatumizi ya bunduki katika matumbawe unasababisha uharibifu mkubwa kwa miamba na inaweza kusababisha ongezeko la ukamataji au vifo vya samaki wachanga.

Uharibifu wa moja kwa moja unaweza kusababishwa na utupaji wa nanga juu ya matumbawe, uvunjaji wa miamba wakati wa kuokota makombe na viumbe wengine ikiwa maji kidogo au mengi, wazamiaji na wavuvi na waogeleaji husimama kwenye miamba na kusababisha uvunjikaji wa miamba hiyo.

Mjadala kuhusu umuhimu wa miamba ya matumbawe hautakamilika bila ya kuangalia vile vile makazi ambayo yanategemeana. Miongoni mwa makazi hayo ni sehemu za mikandaa au mikoko, majani ya baharini na mwani.

Mikoko: Hii ni miti inayohimili chumvi na huota kwenye ukingo baina ya nchi kavu na bahari, nayo iko karibu sana na miamba ya matumbawe. Maumbile yanayotengenezwa kutokana mkusanyiko wa mizizi ya miti hiyo pamoja na aina za mbali mbali za vyakula ni mazalio mazuri ya vijinyama mbali mbali vya baharini ikiwemo vijinyama vya matumbawe. Mbali na faida za moja kwa moja kwa binadamu mikoko ni sehemu za mazalio na malaji kwa aina nyingi za samaki, ni makaazi ya viumbe vya baharini na ni

kinga kwa mawimbi ya moja kwa moja.Utafiti wa kisayansi umethibitisha kuwa jamii ya miti hii inafanya kazi ya kuyachuja na kuyasafisha maji ya bahari kupitia mizizi yake yenye uwezo wa kukamata takataka na sumu zinazopatikana kwenye maji.

Vile vile, namna ya uhusiano uliopo katika mazingira ya jamii za mikoko, ni muhimu sana kwa mazingira mengine ya baharini, kama vile jamii za mwani na majani mengineyo ya baharini. Mwani wa baharini huonekana kwa wingi katika maeneo ya fukwe au juu ya miamba ya matumbawe ambapo mara kwa mara huonekana juu au kufukiwa kutegemeana na mwenendo wa mawimbi ya bahari. Majani bahari, haya huonekana kushikamana pamoja na miamba ya matumabawe katika maeneo yaliyorutubika yakiwa na mizizi na maua yaliyojistawisha kwenye mazingira ya baharini.

Mazingira yote haya yana mahusiano makubwa na miamba ya matumbawe na yanafanyakazi muhimu ya kutengeneza uwiano mzuri wa maisha ya viumbe vya baharini na kuweka mazingira salama ya kuzaliana kwa kila kimoja. Uondoaji na uharibfu wa kimoja kati ya hivyo unaweza kuleta madhara ya hali ya juu kwa viumbe vingine. Haya ni kwa sababu Mwenyezimungu amasema katika Quran:

Katika kuumbwa mbingu na ardhi na mfuatano wa usiku na
mchana ziko hoja za kuonyesha kuwepo kwa Mwenyezi
Mungu mmoja kwa wenye akili. Ambao humkumbuka
Mwenyezimungu wima na wakikaa na kulala na
hufikiri umbo la mbingu na ardhi (pia namna gani
Mwenyezimungu alivyoumba wakasema, Mola wetu
hukuviumba hivi bure.Utukufu ni wako.
Basi tuepushe na adhabu ya moto.
3:190 - 191

## MUHTASARI

Mpango wa Allah Ta'ala, katika uumbaji ni mpango uliotimilia. Ulimwengu ni pahala pa maisha ya viumbe vingi wenye aina tofauti ndani yake. Ameviumba katika kipimo na ulingano maalum na vinaishi katika hali ya uwiano unaobadilika.

Mwanadamu amepewa uwezo wa kufahamu kwa uwazi mahusiano yaliopo baina ya maumbile ya mazingira tofauti na kuweza kutoa ufafanuzi wa hayo.

Kwa vile ulimwengu umeumbwa na kuwekwa katika uwiano na kipimo maalum kinachostahiki, hivyo hivyo, tabia zetu kwa mazingira ya ulimwengu zinatakiwa kuwa za kuangalia kipimo na uwiano muafaka kwa kila kitu.

Hivyo, mara tu tutakapotambua namna ambavyo Allah Ta'ala alivyoumba maumbile tofauti, ni muhimu vile vile kujua majukumu yetu katika kuutunza na kuangalia ulimwengu kwa namna inayoyotakiwa. Hiyo inatubidi kuweka viwango maalum vya matumizi kwa kile tunachokiondoa au kukitumia.

Bahari na viumbe vinavyoishi humo vimeumbwa katika mahusiano yenye kipimo na uwiano ulio mzuri. Hivyo hivyo, Misali imeumbwa ikiwa ni mazingira yaliyo na uwiano timilifu au wenye kujitosheleza.

# SOMO LA NNE - INSAAN

## UJUMBE

Kufahamu lengo la Allah Taala katika kumuumba binadamu linatupa nafasi kujielewa ili tujielewe sisi wenyewe pamoja na kufahamu utukufu wa kazi yake kiujumla kwa ajili ya kuweza kumcha ipasvyo.

## MADHMUNI

Kufikia ufahamu wa nafasi ya binadamu katika uumbaji na umuhimu wa kuhifadhi mazingira.

فِطْرَتَ ٱللَّهِ ٱلَّتِى فَطَرَ ٱلنَّاسَ عَلَيْهَا ۚ

لَا تَبْدِيلَ لِخَلْقِ ٱللَّهِ ۚ

Ndio umbile Mwenyezimungu alilowaumbia watu (yaani dini hii ya kiislamu inawafikiana barabara na umbile la binadamu) Hakuna mabadiliko katika maumbile ya viumbe vya Mwenyezimungu.
30:30

Fitra hali halisi na asili ya maumbile ambayo Allah Taala ameyaumba. Inatupa hisia ya kujua nafasi yetu katika mjumuiko wa viumbe.pamoja na kufahamu mahusiano yetu na mazingira. Baadhi ya wafasiri wametafsiri (fitra) kuwa ni mkusanyiko asilia wa maumbile. Wengine wamefasiri ni kuwa hali asilia na wengine wanafasiri kuwa ni mwenendo wa kimaumbile. Wasomi wa kiilsamu wanakubaliana kuwa neno fitra linamaanisha hali halisi, au hali kiujumla yenye uzuri usio na mipaka ambapo kila kitu ndani ya maumbile kina umuhimu wake wakati tahadhari yake inapaswa kuchukuliwa na kiumbe wa pekee ambae ni mwanadamu.

Mara kwa mara huwa tunasema kuwa watoto wamezaliwa katika hali ya "fitra" isiyo na chembe ya upungufu na safi kabisa. Kama inavyojulikanwa mara nyingi kuwa maana ya Qur'ani iliomo ndani ya lugha ya kiarabu haiwezi kugeuzwa katika maana nyingine na hapa tunaweza kuhitimisha kwa kusema kuwa fitra ni msingi wa kimaumbile wa asili na. Usafi ambao umetumika katika kuumbwa kila kitu wakiwemo wanadamu. Neno fitra ambalo limezalikana katika mzizi wa FTR na linajitokeza mara moja katika Qurani. Pia limejitokeza katika hali ya kitendo chake yani *fatara*, mara kumi na nne. Hali zote mbili za jina na kitendo zimejitokeza kwa pamoja katika hii aya pekee ili kuweza kuleta maana inayostahiki na hisia kamili.

Baadhi ya wafasiri wameita *fitra* kuwa ni umbile halisi, wengine wameita kuwa ni hali asilia au mfano wa asili na wengine kwa kutumialugha nyepesi wameita umbile asilia la ulimwengu.

Fatara inatafsiriwa kwa maana "*kama ilivyoanzishwa au kuumbwa*" ambapo wafasiri wanapojaribu kuleta maana ya aya hii .Kwa ufupi aya hii inatoa ujumbe wa kufahamisha mambo mawili ya msingi. La kwanza hisia ya kujua nafasi yetu katika maumbile aliyoyaumba Allah. Kiuhakika kama walivyo viumbe vingine wanadamu wameumbwa ikiwa ni sehemu ya mkusanyiko wa maumbile asilia aliyoyaumba Allah taala.Mwanadamu ni sehmu ya mkusanyiko wa kimaumbile uliojumuisha vitu vingi ambao hauwezi kubadilshwa.

Jambo la pili ni ujumbe unaoelekeza uwezekano wa kujumuisha pamoja na aya nyengine zinazohusiha uumbaji ambazo zimo ndani ya Qur'an kwa kufahamisha na kuweka misingi thabiti ya dhana ya ekologia ndani ya Din al Islam.

Kufahamika kwa jambo hili huenda ikatuongoza sisi waislamu kutatua matatizo ya kimazingira pamoja na sababu zake za msingi. Qur'an kiujumla inatufahamisha nafasi yetu na mahusiano na ulimwengu kama aya zifuatazo zinavyoonesha.

## AYA ZA ZIADA KUTOKA KWENYE QUR'AN

**Kila kitu kimeumbwa kwa ajili ya mwanadamu -**

هُوَ ٱلَّذِى خَلَقَ لَكُم مَّا فِى ٱلْأَرْضِ جَمِيعًا

Yeye ndiye aliekuumbieni vyote vilivyomo katika ardhi.
2:29

**Uumbaji wa mbingu na ardhi ni mkubwa kuliko watuz -**

لَخَلْقُ ٱلسَّمَٰوَٰتِ وَٱلْأَرْضِ أَكْبَرُ مِنْ
خَلْقِ ٱلنَّاسِ وَلَٰكِنَّ أَكْثَرَ ٱلنَّاسِ لَا يَعْلَمُونَ

Kwa yakini umbo la mbingu na ardhi ni kubwa kuliko umbo la wanadamu. Lakini watu wengi hawajui.
40:57

**Kuna makusudio katika uumbaji -**

وَمَا خَلَقْنَا ٱلسَّمَآءَ وَٱلْأَرْضَ وَمَا بَيْنَهُمَا بَٰطِلًا

Na hatukuziumba mbingu na ardhi na vilivyomo ndani yake bure.
38:27

**Kuumbwa ni kwa ajili ya kupewa mtihani -**

وَلَوْ شَآءَ ٱللَّهُ لَجَعَلَكُمْ أُمَّةً وَٰحِدَةً وَلَٰكِن لِّيَبْلُوَكُمْ فِى مَآ

ءَاتَىٰكُمْ فَٱسْتَبِقُوا۟ ٱلْخَيْرَٰتِ

Na kama angalitaka Mwenyezimungu angalikujaalieni umma (jamii)
mmoja lakini alikutieni mtihani kwa yale aliokupeni.
Tangulieni katika wema.
5:48

**Maumbile ya dunia si uwanja wa mchezo -**

وَمَا خَلَقْنَا ٱلسَّمَآءَ وَٱلْأَرْضَ وَمَا بَيْنَهُمَا لَٰعِبِينَ

Na hatukuziumba mbingu na ardhi na
vilivyomo baina yake kwa mchezo.
21:16

**Vipo viumbe vingine kama wewe -**

وَمَا مِن دَآبَّةٍ فِى ٱلْأَرْضِ وَلَا طَٰٓئِرٍ يَطِيرُ
بِجَنَاحَيْهِ إِلَّآ أُمَمٌ أَمْثَالُكُم

Na hakuna mnyama katika ardhi wala ndege arukaye kwa mbawa zake
mbili ila ni umati kama nyinyi.
6:38

**Vile Vile zinagatia -**

Na hakika tumewatukuza wanadamu na tumewapa vya kupanda bara na baharini, na tumewaruzuku vitu vizuri vizuri na tumewatukuza kuliko wengi katika wale tuliowaumba, kwa utukufu ulio mkubwa(kabisa) - 17:70.

Je huoni kwamba Mwenyezimungu amevitiisha kwa ajili yenu vilivyomo ardhini na amekutiishieni marekebu zinazopita baharini kwa amri yake - 22:65

MwenyezuiMungu ndie aliekutiishieni bahari ili humo zipite marikebu kwa amri yake, na ili mtafute fadhila zake na mpate kushukuru - 45:12.

## MAZINGATIO ZAIDI

Binadamu ni kiumbe mwenye akili na mwenye mkusanyiko wa mambo mengi katika mfumo wa uumbaji wa Alla Taala. Lengo letu kuu ni kumtumikia Muumba kwa kutambua nafasi yetu ya pekee katika maumbile haya ya kuvutia. Sisi ni viumbe wa aina ya peke yake kwa kuwa kila kitu kiliumbwa kwa ajili yetu (2:29) na bado vile vile ni wa daraja ya chini kabisa " uumbwaji wa mbingu na ardhi kukubwa kuliko maumbile ya kuumbwa kwa binadamu" (40:57).

Wanadamu ni wenye uwezo wa kufanya mabadiliko katika baadhi ya harakati na mifumo ya kimaumbile kuliko wanavyoweza kufanya viumbe vyengine. Tunatumia akili zetu tulizopewa na Allah Taala na kubuni vitu vinavyofanya maisha kuwa mazuri kwetu. Tumeweza kutumia upepo na moto na tunaweza kusimamisha, na kubadilisha au kuelekeza mito mikubwa kwenda sehemu nyengine au kujenga mabwawa makubwa makubwa. Hata hivyo, hivi sasa, watu wameanza kutambua kuwa huenda tunafanya shughuli hizi kupita viwango vinavyostahiki na matokeo yake kuanza kutishia uhai na maisha vizazi vinavyotarajiwa baadae.

Ingawaje wanadamu ni wa mwisho katika mpangilio wa uumbwaji, lakini tumebaki kuwa ni viumbe pekee tuliopewa fursa nzuri (17:70) kuliko baki ya viumbe wengine ambao wamedhalilishwa kututii sisi (22:65). Tunakumbushwa kuwa ipo jamii nyengine ya viumbe ambapo dhamana ya kuiangalia ipo mabegani mwetu. Lakini vitendo vyetu vinaonesha kuwa hatuna mwamko wa kuyajua majukumu au dhamana zetu na vile vile nafasi yetu katika *fitra* ya Allah Taala.

Kila tunachokiona basi ni *n'ihma* (neema) aliyotupa Allah Ta'ala. Hata hivyo, neema hiyo imewekewa masharti maalum. Dunia ni mahali petu

pa kufanyiwa mtihani ambao ni kipimo cha *ihsan* (matendo mema katika ibada) kwa maana iliyo pana, ni namna ya kuishi kwa jinsi Mwenyezimungu (SW) anavyopendelea. Hivyo, kila tulifanyalo inatupasa kuzingatia maisha ya mshikamano wa mazingira yetu ya ndani na nje.

## MAHUSIANO NA MAZINGIRA YA BAHARI

Bila ya shaka, yapo mahusiano makubwa baina yetu na mazingira ya bahari. Bahari ni makaazi ya samaki tunaowala, Mwenyezimungu SW amesema yeye ndiye aliekuumbieni vyote vilivyomo katika ardhi (2:29). Bahari vile vile, inatusaidia kufanya safari zetu, Mwenyezimungu Mtukufu ameifanya bahari kuwa ni tiifu kwetu (45: 12) kwani tunaitumia kupitishia vipando kwenda Unguja, Pemba, Tanzania bara au sehemu nyengine ulimwenguni. Vile vile, katika matukio tofauti vile vile tunaitumia kwenda Kisiwa cha Misali kuvua kwa ajili ya kupata mahitaji yetu. Kwa upande mwengine bahari inasaidia katika kubadilika kwa hali ya hewa kwa ajili ya ufanyikaji wa mvua zinazosaidia urutubishaji wa ardhi na ukuzaji wa mazao yetu.Yote haya hufanyika katika ardhi hii.

Aidha, Bahari inaficha siri nyingi katika kina chake. Humo ndimo kwenye maisha ya miamba ya matumbawe ambamo yamechukua maelfu ya miaka katika ukuaji wake na kuwa makaazi ambayo samaki wanaoishi na kuzaliana na hivi sasa wanadamu tunafaidika kwa kiwango kikubwa kabisa.

## MUHTASARI

Kiukweli wanadamu ni viumbe wenye bahati kubwa, fursa ambayo hapana kiumbe chengine kilichopewa ndani ya ulimwengu huu. Tukiangalia aya zililizotajwa hapo juu, tunaona kuwa sisi ni viumbe tuliopewa upendeleo ambapo kila kitu kimeumbwa kwa ajili yetu na vikadhalilishwa kwetu. Tumetukuzwa na Allah Taala kwa kupewa kipaji cha elimu, nguvu, maarifa, uwezo wa kupambanua lililo jema na ovu pamoja na kuamua au kuchagua la kuliendea, na vyote hivi ni sehemu ya ubingwa wake wa hali ya juu.

Binadamu ni wa pekee ambae Allah Ta'ala amempa akili na wingi wa fursa na wenye kuhusika zaidi katika mfumo huu mkubwa wa kimaumbile.

Ni sehemu muhimu ya Ulimwengu na tumejumuishwa katika *fitra*, ndani ya mfumo wa kimaumbile.Ingawaje uumbaji wa baki ya viumbe ni mkubwa kuliko uumbwaji wa wanadamu (40:57) lakini kila kitu kimeumbwa kwa ajili ya matumizi yetu (2:29). Lengo la kuwepo kwetu juu ya mgongo wa ardhi ni kupewa mtihani au kupimwa kiwango chetu cha utekelezaji wa ibada hiyo kwa ukomo wa uwezo wetu pamoja na kushindana baina yetu katika kufanya wema (5:48).

## SOMO LA TANO - FASAD

### UJUMBE

Pamoja na uwezo aliopewa mwanadamu wa kufikiri na kuchanganua pamoja na kuamua mambo, hata hivyo anatumia akili, maarifa na uwezo aliopewa katika kufanya - fasad- kuharibu na kuangamiza mazingira anayoishi na kuyategemea kuendeleza uhai wake.

### MADHUMUNI

Kufahamu uwezo wa mwanadamu katika kusababisha uharibifu na matokeo yake yake.

ظَهَرَ ٱلْفَسَادُ فِى ٱلْبَرِّ وَٱلْبَحْرِ بِمَا كَسَبَتْ
أَيْدِى ٱلنَّاسِ لِيُذِيقَهُم بَعْضَ ٱلَّذِى عَمِلُوا۟ لَعَلَّهُمْ يَرْجِعُونَ

Uharibifu umedhihiri bara na baharini kwa sababu ya yale
yaliofanya na mikono ya watu ili awaonjeshe (adhabu)
ya mambo (maovu) waliyoyafanya. (Kwani) Huenda wakarejea
(wakatubia) kwa Mola wao
30:41

Mazungumzo mengi hivi sasa yameelekezwa katika suala la jinsi mwanadamu anavyosahau jukumu lake la Khalifa (tutazungumzia katika somo linalofuatia) kiasi ambacho viumbe sisi tumedharau dhamana zetu ndani ya fitra ya Allah Ta'ala. Vipo viwango maalum vya kuendelea kutumia maliasili kulingana na umuhimu wa jambo. Hata hivyo kwasababu

ya uchache wa raslimali zilizopo, lakini tunachukua tahadhari ndogo kwa maafa yanayoweza kutokea kutokana na matendo yetu.

Tunachafua hewa tunayoivuta na maji tunayokunywa ambapo kiwango cha uchafuzi kimefikia hali ya kutisha, na sasa maafa makubwa yanaelekea upande wetu katika kuharibu afya zetu. Wanasayansi wamethibitisha kwamba vitendo vyetu vimechangia mabadiliko makubwa ya hali ya hewa katika sayari yetu hii ya pekee ambayo tunaitegemea kwa maisha yetu.

## AYA ZA ZIADA KUTOKA KWENYE QUR'AN

**Msifanye ubadhirifu, fujo (ufisadi, uharibifu) –**

كُلُوا۟ مِن ثَمَرِهِۦٓ إِذَآ أَثْمَرَ وَءَاتُوا۟ حَقَّهُۥ يَوْمَ
حَصَادِهِۦ ۖ وَلَا تُسْرِفُوٓا۟ ۚ إِنَّهُۥ لَا يُحِبُّ ٱلْمُسْرِفِينَ

Kuleni matunda yake wakati yanapokuwa tayari na toeni haki yake siku ya kuvunwa kwake na msitumie kwa fujo, hakika yeye Mwenyezimungu hawapendi wanaofanya
fujo. 6:141

**Na msivuke viwango –**

يَٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُوا۟ لَا تُحَرِّمُوا۟ طَيِّبَٰتِ مَآ أَحَلَّ ٱللَّهُ لَكُمْ
وَلَا تَعْتَدُوٓا۟ ۚ إِنَّ ٱللَّهَ لَا يُحِبُّ ٱلْمُعْتَدِينَ

Enyi mlioamini musiharamishe vizuri alivyokuhalalishieni Mwenyezimungu, wala msivuke mipaka. Hakika Mwenyezimungu hawapendi warukao mipaka.
5:87

**Mwandamu hasimu mkubwa (wa wazi) –**

خَلَقَ ٱلْإِنسَٰنَ مِن نُّطْفَةٍ فَإِذَا هُوَ خَصِيمٌ مُّبِينٌ

Amemuumba Mwanadamu kutokana na manii tena
amekua hasimu mkubwa (mbishi)
16:4

**Vile vile zinagatia –**

Na kwa hakika tumekumakinisheni (tumekukalisheni) katika ardhi na tumekuwekeeni humo vitu vinavyo hitaji maisha yenu ni shukrani chache tu mnayomshukuru - 7:10

Wala msifanye uharibifu katika nchi baada ya kuwa imekwisha kutengenezwa.na muombeni kwa kuogoba na kutumaini. Bila shaka rehema ya Mwenyezimungu iko karibu sana na (Wale waja wake) wanaofanya wema - 7:56

Jee huoni kwamba Mwenyezimungu ameziumba mbingu na ardhi kwa haki? Akitaka atakuondoweni mara moja na kuleta viumbe (wengine) wapya na hilo kwa Mwenyezimungu si gumu - 14:19

## UFAFANUZI ZAIDI

Zawadi ya akili (ujuzi) ambayo Allah Taala ametupa inaweza ikatumika kwa kusababisha matukio mazuri au mabaya kama ya uharibifu. Tunatumia maarifa yetu kuchanganua juu ya matendo mabaya na kutaka msamaha kwa matendo yetu maovu. Uharibifu na uchafuzi wa mazingira tunaoufanya kwa mazingira ya bara na baharini pamoja na vita tulivyotangaza dhidi ya viumbe hai ni ushahidi wa kiza kilichotanda kwenye maumbile yetu. Tabia ya uharibifu aliyonayo mwanadamu si kitu kipya lakini kuishi katika *fitra* kunatutambulisha kila wakati kuwa, makovu ambayo tumeyasababisha katika ulimwengu asilia yatachukua muda mkubwa kuweza kupona.

Mazingira ni kama mwili wa mwandamu, vijeraha vidogo vidogo huchukua muda kupona na hatimaye kuacha mwili pasina kuwa na kijeraha, majeraha mengine hupona lakini huacha alama ya makovu; majeraha makubwa husababisha hali isiyokuwa ya kawaida kwenye mwili kama ulemavu au banguzi. Kwa hiyo husababisha athari ya kudumu katika maumbile ambayo ambayo mwili hufanyakazi.

Hii leo tunaishi nje ya *fitra* na tunajua hatuna viwango vya kukadiria. Tumekuwa wabadhirifu au wenye kufanya fujo (6:141), kwa maana tumekithirisha ubinafsi na uharibifu. Matukio makubwa ya uharibifu ulimwenguni yametokea katika kipindi cha miaka mia au zaidi iliyopita. Lakini kinachofanyika kwenye kisiwa cha Misali ni cha matukio ya hivi karibuni mno. Wazazi wetu hawakuwa na matatizo haya. Katika nyakati zao, hayakusikilikana matukio ya uharibifu wa kupindukia wa maliasili za baharini, mbinu za uvuvi zisizofuata taratibu, uvuvi wa aina adimu za viumbe pamoja na uharibifu wa maeneo ambayo viumbe vya baharini vinazaliana. Basi ikiwa watatokea kuishi hii leo, basi watashangazwa na kuchangnyikiwa.

## MAHUSIANO NA MAZINGIRA YA BAHARI

Misali kama ilivyo hivi sasa inaelekea kwenye hali ya kutisha.Hii inatokana na matukio mbali mabali ya uvuvi usiofuata taratibu kama vile matumzi ya baruti,utupaji nanga bila tahadhari kwenye matumbawe, ukusanyaji na matumizi ya matumbawe kwa ajili ya kuchoma chokaa, matumizi ya sumu kwa kuvulia pamoja na matumizi ya njia nyengine zinazoleta athari mbaya. Kuharibu matumbawe ni sawa na mwenye kutupa au kulenga baruti kwenye mwembe kwa ajili ya kupata embe au hata kuukata mwembe wenyewe.Hivyo hautobakia mwembe wala embe, halkadhalika hali hiyo vile vile ni sawa na matumbawe na samaki.

Hii ni tabia isiyokubalika ambayo inaathiri mfumo wa kiekologia ambao hatimaye unapelekea upotevu wa samaki pamoja na aina za viumbe wengine adimu wa baharini.

Ni kweli kuwa, ikiwa hatutabadilisha tabia zetu kuelekea kwenye matumizi mazuri ya maeneo ya kisiwa cha Misali, basi tutaweza kushuhudia kupotea kwa aina mbali mbali za samaki ambao tunawategemea kwa chakula na maisha yetu.

## MUHTASARI

Kiukweli tumo katika tabia ya kuhujumu makaazi tunayoyategemea ambayo yanatuwezesha kuendeleza uhai wetu. Mwenyezimungu mtukufu ametukumbusha kuwa yeye ni mwenye huruma na viumbe na akatuhimiza tuwe na tabia ya kujali maisha yetu na viumbe wengine wanaoishi ardhini; kwa kutoyawachia mazingira yajiboreshe (27:64); tunakuwa mahasimu wakubwa (16:4); lakini Allah Ta'ala anajua namna gani ya kutuadhibu.

# SOMA LA SITA - KHALIFA

## UJUMBE

*Khalifa* wa Allah Ta'ala's (Wakala wa Allah, Mwangalizi, mrithi, mwenye kufata badala ya waliopita) katika ulimwengu. Sisi ni mawakala na waangalizi wa ulimwengu. Hivyo tunalazimika kutunza mazingira na wala siyo kuyaharibu.

## MADHUMUNI

Kufahamu majukumu yetu ya uongozi wa ulimwengu na namna gani tunapaswa kuwajibika kufanya kwa viumbe vingine vilivyo tofauti na sisi.

Kufikia ufahamu wa dhamana ya kila mmoja katika kutimiza jukumu la uwakala kwa raslimali za ulimwengu.

## AYA ZA MSINGI KWENYE QUR'AN

وَهُوَ ٱلَّذِى جَعَلَكُمْ خَلَٰٓئِفَ ٱلْأَرْضِ

Naye ndiye aliyekufanyieni washikaji wa mahala pa hao
waliondoka katika ardhi.
6:165

Mwenyezimungu Mtukufu amemtukuza mwanadamu kwa kumfanya kuwa khalifa na amempa jukumu la kusimamia na kuendeleza mazingira na kuhifadhi rasilimali zake kwa faida ya wakazi wote wa sayari hii. Kama tulivyoona kuwa mwanadamu ana nafasi muhimu katika mipango ya maumbile ya Allah Taala. Ametupa zawadi ya akili au maarifa pamoja na neema nyingi, vile vile ametupa jukumu kwa kutufanya viongozi, walinzi wa mazingira aliyotuumbia.

Tumeona katika somo la *insan* (katika kurasa zilizotangulia) kuwa uumbwaji wa kila kitu ni mkubwa kuliko sisi. Pamoja na hayo, tumepewa jukumu la *Ukhalifa*. Amana kubwa ipo juu ya mabega yetu. Tumeamrishwa kuwa waadilifu kwa baki ya viumbe wake. Tutaangalia namna ya majukumu haya mawili ya ziada yanavyoendana na dhamana ya *Ukhalifa* katika sehemu hii.

## AYA ZA ZIADA KWENYE QUR'AN

**Amana kubwa imewekwa katika mikono yenu –**

إِنَّا عَرَضْنَا ٱلْأَمَانَةَ عَلَى ٱلسَّمَٰوَٰتِ وَٱلْأَرْضِ
وَٱلْجِبَالِ فَأَبَيْنَ أَن يَحْمِلْنَهَا وَأَشْفَقْنَ مِنْهَا وَحَمَلَهَا
ٱلْإِنسَٰنُ إِنَّهُۥ كَانَ ظَلُومًا جَهُولًا

Kwa yakini sisi tulizidhihirisha amri zetu na makatazo yetu (tukaziuliza) mbingu na ardhi na milima (kuwa zitachukuwa madaraka ya kufuata amri hizo na kujiepusha na makatazo hayo vikakataa) lakini mwanadamu akachukuwa. Bila shaka yeye ni dhalimu mkubwa, mjinga sana.
33:72

**Vile vile zinagatia –**

Wakasema Malaika, utaweka humo watakaofanya uharibifu humo na kumwaga damu - 2:30

Hakika Mweyezi Mungu amekuamrisheni kuzirudisha amana kwa wenyewe(wanaostahiki) Na mnapohukumu baina ya watu mhukumu kwa haki - 4:58

Na hatukuumba mbingu na ardhi na vilivyomo ndani yake ila kwa ajili ya (kudhihirisha) haki 15:85

Enyi mlioamini! Kuweni wenye kusimamia uadilifu, mtoapo ushahidi kwa ajili ya Mwenyezimungu ijapokuwa ni juu ya nafsi zenu(au juu) ya wazazi (wenu) na jamaa zenu akiwa tajiri au masikini. Mwenyezimungu anawastahikia zaidi(kuliko wewe) - 4:134

Enyi mlio amini msimfanyie khiana Mwenyezimungu na Mtume wake, wala msikhini amana zenu na (hali mnajua kuwa ni vibaya hivyo) - 8:27

Kisha tukakufanyeni nyinyi kuwa makhalifa (wenye kushika nafasi) (kurithi) mahala pao katika ardhi ili tuone jinsi mtakavyofanya - 10:14

Kwa hakika Mwenyezimungu anaamrisha uadilifu na kufanya ihsani - 16:90

## UFAFANUZI WA ZIADA

*Kazi ya Ukhalifa* ni jukumu alilotupa Allah Taala.Kuchunga Amana ni kielelezo cha kutambulika dhamana hii. Uadilifu ni jambo la msingi la kuliangalia katika kutekeleza amana tuliyopewa.

Jukumu ya Ukhalifa ni dhamana kubwa aliyopewa mwanadamu ambapo hakuna kiumbe yeyote mwingine alieweza kuichukua. Ufafanuzi wa kiwango cha ukweli huu kinaelezwa wakati "Ardhi, mbingu na majabali yalipokataa kuchukua amana hii. "(angalia sura ya 33:72).

Wanadamu wanahitajika kujali na kusimamia Dini ya Allah ili iweze kuthibitisha kuwa ni utaratibu sahihi wa maisha ya mwanadamu (33:72). Akili ya kibinadamu yaweza kushangaa kuona kuwa kile kilichosemwa ndani ya Qur'an "*kuumbwa kwake si kukubwa kuliko umbile la mbingu na ardhi*" na baadae kupewa jukumu zito la kuangalia viumbe wengine. Basi wanadamu twahitajka kuonyesha shukurani kutokana na zawadi ya akili na maarifa aliyotupa Allah .

Ikiwa kama *Khalifatullah* (wakala wa Allah Ta'ala) mwanadamu anahitajika kufanya kazi ya kuutunza na kuusimamia ulimwengu ili uendelezwe katika utaratibu unao endana na makusudio ya uumbaji. Nao ni kuutumia kwa busara na kwa faida yetu bila ya kusababisha madhara kwa viumbe wengine wanaoishi katika sayari hii. Hii ni kuitekeleza amana iliyopo mikononi mwetu kwa kuzingatia mipaka ya fitra.

Mamlaka tuliyonayo juu ya baki ya maumbile sio fursa ya kufanya tunavyotaka bali ni dhamana au jukumu, ambapo linachukua mzigo wa uwajibikaji. Kipimo cha uwajibikaji wetu kitapimwa kwa matendo ya uadilifu na huruma kwa makusudio ya kufanya mema kila wakati. Hiyo ni *ihsan*, kufanya yale yanayompendezesha Allah ambaye yupo daima na anatuona kila saa na kila wakati. Hivyo, hakuna cha kufanya zaidi ya kufanya ihsaan –

هَلْ جَزَآءُ ٱلْإِحْسَٰنِ إِلَّا ٱلْإِحْسَٰنُ

Hakuna malipo ya Ihsani isipokuwa kulipa Ihsani (Vile vile)
55:60

Mwenyezimungu Mtukufu ameumba kila kitu katika umbile lake na baadae akakiongoza kwenye utaratibu wa kufata (20:50). Maelekezo ya msingi ya maisha yake yamebainishwa kwa uwazi ndani ya Quran. Uhifadhi katika Uislamu unafahamika kuwa ni sehemu ya tabia njema ambayo inatuelekeza jinsi gani tutayaendesha mambo yetu na kuyasimamia. Hii sio kazi ya mtu mmoja bali ni jukumu la kila mtu kuhakikisha kuwa tabia njema zinahamasishwa na kuelekezwa kufatwa na tabia mbaya zinakatazwa. Allah taala anatwambia katika Qur'an: –

وَلْتَكُن مِّنكُمْ أُمَّةٌ يَدْعُونَ إِلَى ٱلْخَيْرِ وَيَأْمُرُونَ بِٱلْمَعْرُوفِ
وَيَنْهَوْنَ عَنِ ٱلْمُنكَرِ ۚ وَأُو۟لَٰٓئِكَ هُمُ ٱلْمُفْلِحُونَ

Na wawepo katika nyinyi watu wanaolingania kheri
(utaratibu wa maisha ambao Allah ameuridhia)
na wanaoamrisha mema na wa kukataza maovu.
Na hao ndio watakaotengenekewa.
3:104

## MAHUSIANO NA MAISHA YA BAHARINI

Yale yanayotutafautisha na baki ya viumbe wengine ni kwamba sisi tutawajibika kwa kuhesabiwa kutokana na matendo yetu. Uwajibikaji huu unatutaka tuchukuwe hatua za dharura na za makusudi katika kuyatunza vizuri mazingira yetu ya Kisiwa cha Misali.

Kwa vile sisi ni mawakala wa Allah Taala katika ulimwengu, basi tunayo majukumu mazito kwa maisha ya viumbe vya baharini hasa katika kuhifadhi kisiwa hicho ili paendelee kuwa pahala penye uzuri wa kipekee pamoja na mshikamano wa kiekologia kwa ajili ya kusaidia maisha yetu.

- Mazingatio yetu makuu lazima yawe kwenye matumizi mazuri ya maliasili za baharini na kuhifadhi mfumo mzima wa kiekologia kwa faida ya vizazi vyote.
- Nyakati zote lazima tutumie zana za uvuvi ambazo zinaendana na maadili ya uhifadhi.
- Maeneo muhimu ambayo samaki wanazaliana (tengefu) ni vizuri yakaachwa kutumiwa ili kuboresha upatikanaji wa samaki kwa sasa na siku za baadae.
- Aina za viumbe walio hatarini kutoweka kama vile kasa, pomboo, nguva, makome makubwa, majongoo na wengineo kama hao ni busara wakaachwa bila ya kuvuliwa ili waendelee kuzaliana kwa faida ya wote.
- Kwa ujumla kila aina ya tahadhari inahitajika kuchukuliwa wakati watu wanapofanya kazi katika mazingira nyeti ya sehemu zilizohifadhiwa.

## MUHTASARI

Kutokana na hekima na busara zake, Allah Taala, amemchagua mwanadamu kuwa Khalifa (*wakala wake*) na kumpa jukumu la uangalizi wa dunia tunayoishi. Katika kufanya haya vile vile, amemtunukia mwanadamu akili ya kuweza kupambanua mema kutokana na mabaya. Mwenyezimungu ameweka amana kwenye mabega yetu na ametukumbushia kuitekeleza kwa kuangalia uadilifu na usawa wa haki za kila kiumbe. Kipaumbele chetu katika haya hivi sasa, ni kutumia uwezo huu na kutekeleza majukumu haya sio tu katika kulinda na kuhifadhi maeneo ya Hifadhi ya kisiwa cha Misali kwa manufaa ya viumbe vyote, bali vile vile, mazingira mengine katika kila pembe ya maisha yetu.

# HITIMISHO

Tukiangalia mfano wa Misali, ni sehemu tu ya alama au dalili za uweza wake Mwenyezimungu. Vile vile kielelezo cha mizan (uwiano, kipimo halisi cha uumbaji) vile vile ni sehemu ya *fitra* (umbile) alilotuumbia Muumbaji. Hapo sio mahala pa mchezo bali ni sehemu zinazotoa huduma endelevu kwa watu wa Pemba. Misali vile vile ni sehemu ya Uislamu kwa kule kusalimu amri kwa Muumba na ni mfano wa namna maumbile yalivyowekwa kufanya kazi.

Kwa waislamu, hii inaonyesha uwezo wa Allah katika uumbaji na ni mfano tosha wa vipi maumbile yamewekwa ili yaweze kufanya kazi inayotarajiwa. Itakua ni sahihi kabisa tukisema kwamba hii ni neema aliyotoa Mwenyezimungu kwa watu, ambao wanategemea katika maisha na maendeleo yao.

Tutashindwa kufaulu mtihani wa amana tuliyopewa na Allah Tala katika kutekeleza jukumu la Ukhalifa ikiwa hatutakuwa waadilifu kwa kutumia maarifa na akili zetu katika kufanya maamuzi ya matumizi ya rasilimali hizo. Au badala yake kusababisha *fasad* (uharibifu) kiasi ambacho tutafanya vizazi vijavyo kukosa manufaa yake. Qurani inafupisha habari yote kwetu kama ifuatavyo:

وَٱللَّهُ أَنزَلَ مِنَ ٱلسَّمَآءِ مَآءً فَأَحْيَا بِهِ ٱلْأَرْضَ بَعْدَ مَوْتِهَآ ۚ إِنَّ فِى ذَٰلِكَ
لَءَايَةً لِّقَوْمٍ يَسْمَعُونَ ﴿٦٥﴾ وَإِنَّ لَكُمْ فِى ٱلْأَنْعَٰمِ لَعِبْرَةً ۖ نُّسْقِيكُم مِّمَّا
فِى بُطُونِهِۦ مِنۢ بَيْنِ فَرْثٍ وَدَمٍ لَّبَنًا خَالِصًا سَآئِغًا لِّلشَّٰرِبِينَ ﴿٦٦﴾
وَمِن ثَمَرَٰتِ ٱلنَّخِيلِ وَٱلْأَعْنَٰبِ تَتَّخِذُونَ مِنْهُ سَكَرًا وَرِزْقًا
حَسَنًا ۗ إِنَّ فِى ذَٰلِكَ لَءَايَةً لِّقَوْمٍ يَعْقِلُونَ ﴿٦٧﴾ وَأَوْحَىٰ رَبُّكَ إِلَى ٱلنَّحْلِ
أَنِ ٱتَّخِذِى مِنَ ٱلْجِبَالِ بُيُوتًا وَمِنَ ٱلشَّجَرِ وَمِمَّا يَعْرِشُونَ ﴿٦٨﴾ ثُمَّ كُلِى

مِن كُلِّ ٱلثَّمَرَٰتِ فَٱسۡلُكِي سُبُلَ رَبِّكِ ذُلُلٗاۚ يَخۡرُجُ مِنۢ بُطُونِهَا
شَرَابٞ مُّخۡتَلِفٌ أَلۡوَٰنُهُۥ فِيهِ شِفَآءٞ لِّلنَّاسِۚ إِنَّ فِي ذَٰلِكَ لَأٓيَةٗ لِّقَوۡمٖ
يَتَفَكَّرُونَ

Na MwnyeziMungu ameteremsha maji kutoka mawinguni, na kwa hayo akaihuisha ardhi baada ya kufa kwake. Kwa hakika, katika hayo imo ishara - dalili ya wazi- za (uwezo wake) kwa watu wenye kusikia (wenye kutaka kufahamu na kuchanganua mambo na baadae kuagalia ya kuyafata).
Na bila ya shaka katika wanyama muna mazingatio makubwa kwa ajili yenu; Tunakunywisheni katika vile viliomo matumboni mwao (vikitokea) baina ya choo na damu (nayo ni maziwa) tunakunywisheni maziwa safi na mazuri kwa wanywao.
Na katika matunda ya miti ya mitende na mizabibu mnatengeneza vinyweo vya vilevi (vinavyokatazwa) na mnapata riziki nzuri (vile vile). Hakika katika haya muna mazingatio makubwa kwa watu watumiao akili zao.
Na mola wako akamfahamisha (akamuongoza) nyuki ya kwamba "jitengezee majumba (yako) katika milima na katika miti na katika majumba wanayojenga (watu). Kisha kula katika kila matunda na upite katika njia za Mola wako zilizofanywa nyepesi (kuzipita)". Kinatoka katika matumbo yao kinywaji (asali) chenye rangi mbali mbali, ndani yake mna ponyo (poza) kwa wanadamu. Hakika katika hayo muna mazingatin makubwa kwa watu wenye fikra (wenye kuzingatia)
16: 65 – 69

# MANENO YA HITIMISHO

Qur'an tukufu imebeba ujumbe mzito unaoelimisha kuhusu misingi ya utunzaji wa mazingira ambao kwa kiasi kikubwa unatilia mkazo ufahamu wa umuhimu wa maumbile ambayo Allah taala ameyaumba. Utunzaji wa mazingira ikiwemo maliasili zake, ni jukumu la kidini ambalo kila muislamu anastahiki kuwajiika nalo. Viongozi wa dini ni lazima wachukue juhudi za kila aina kuhakikisha wanaelimisha jamii wanazoziongoza juu ya mafunzo ya Qur'an yanayohusiana na maliasili na mazingira kiujumla. Pamoja na hayo, wanahitajika kutoa miongozo inayostahiki kwa kila mmoja kushiriki katika uhifadhi wa mazingira

Uharibifu na uchafuzi mkubwa wa mazingira unatokana na watu kutofahamu pamoja na kudharau mambo ambayo Allah Taala amewawajibisha kuyafanya. Kwa hali hiyo ni muhimu kwa kila muislamu kuzingatia yafuatayo -

- Uhifadhi au utunzaji wa mazingira ni jukumu la kidini ambalo Allah SW ametutaka kuliangalia kwa makini. Uharibifu wowote wa makusudi wa mazingira na maliasili yake ni aina ya ubadhirifu ambao ambao Allah Taala ameukataza ndani ya dini ya kiislamu.
- Utumiaji wa fujo pamoja na wa kupita mipaka umekatazwa kabisa ndani ya Uislamu.
- Kila mmoja lazima azingatie maendeleo endelevu ya ulimwengu kwa kuhakikisha matumizi mazuri na ya busara pamoja na kuheshimu maisha ya viumbe wengine.

Kila mwanadamu ni mlinzi wa mazingira yake na ni lazima afanye kila aina ya jitihada kuwaelimisha wengine na kuhakikisha kuwepo kwa mazingira yaliyo salama sio kwa yeye peke yake bali kwa kila kiumbe wa ulimwengu huu wa sasa na baadae. Kabla ya kuhitimisha maneno haya, haitakuwa busara ikiwa sitoainisha shukrani na kuridhika kwangu kwa msaada na ushauri wa kielimu na michango mbali mbali niliyoipata kutoka kwa watu wafuatao; pamoja na wale ambao wametajwa mwanzoni mwa kiitabu hiki, shukrani ni kwa masheikh, wanachuoni na watu binafsi wakiwemo, Al- Marhum

sheikh Ali bin Seif wa Zanzibar, Sheikh Moh'd Suleiman wa Jumuiya ya Istiqama Chake Chake Pemba pamoja Ustaadh Talib Juma Ali wa African Muslim Agency Zanzibar katibu wa Mufti Tanzania Sheikh Abdulshakur Dr. Bakari S. Asseid-Mkurugenzi wa Idara ya Mazao ya Biashara, Matunda na Misitu Zanzibar na Hajj Mohammed Hajj wa Jumuiya ya Mazingira Wete Pemba..

Vile vile ile vile Sitoacha kushukuru msaada na mashirikiano ya dhati niliyoyapata kutokana na wafanyakazi wa shirika la kimataifa la CARE katika Tanzania, WWF for living planet (TZ), Mradi wa Menai Bay, Idara ya Mazao ya Biashara, Matunda na Misitu, Zanzibar na Idara ya Uvuvi Zanzibar. Nawashukuru wote kwa msaada binafsi na wa kiutawala na kwa kuelewa umuhimu wa Muongozo huu. Mwishowe sitosahau kuwashukuru familia yangu hasa Bibi Aisha na Mtoto Fazlun kutokana na ustahamilivu na kunipa nguvu katika kila hatua za matayarisho ya kitabu hiki.

Wote hawa pamoja na niliowaacha kuwataja, nawaombea Allah awape kila la kheri hapa duniani na kesho Akhera.

Wabillahi Tawfiq

Ali Kh. Thani
Mratibu wa Mawasiliano, Uenezi na Mafunzo
Programu ya WWF –RUMAKI, Tanzania

Mwanzoni alikuwa

Afisa Elimu ya Mazingira kwa maadili ya Kiislamu.
Mradi wa Misali – uliosimamiwa na CARE Tanzania
Jauary, 2008

## BAADHI YA HADITHI ZA S.A.W

Ingawaje zipo hadithi nyingi tu zinazohusiana na uhifadhi wa mazingira, lakini hapa tumejaribu kuzitaja baadhi yake tu. Wataalamu wanaweza kufanya juhudizaidi katika kutafuta na kuoanisha hadithi na masomo tofauti.

- Kila kiumbe kinamtegemea Mwenyezimungu na Mwenyezimungu humpenda zaidi yule mbae anaevifanyia wema vinavyomtegemea yeye.(Kash-al-Khafa)

- Yeyote atakaepanda mti na baadae akauangalia kwa kuutunza hadi kukua kwake hatimae vikafaidika viumbe vyengine kutokana na matunda yake, basi mtu huyo ataandikiwa thawabu (wema) na Mwenyezimungu. (Bukhari and Muslim)

- Imesimuliwa kutoka kwa Bw. Jar'ir bin Abdullah Al- Bajali (RA) kuwa amesema mjumbe wa Mwenyezimungu kuwa, Ambae hawarehemu wenziwe (kuvionea huruma viumbe vyenzake) nae hatarehemewa na Mwenyezimungu.". (Sahihi-Al Bukhari, Hadithi ya: 2020- 8:42)

- Hakika Mwenyezimungu anapendelea (anathamini na kuhimiza uadilifu au kufanya wema katika mambo yote). Hivyo mtakapochinja chinjeni kwa vizuri kwa kuvinoa vizuri visu vyenu kabla ya kuchinja ili mumpe nafuu mnyama.

- Imepokewa kutoka Kwa Bw. Anas Ibn Malik (RA), Alisema Mtume wa Mwenyezimungu, atapopanda mti muislamu yoyote na baadae binadamu au mnyama akala au akafaidika kutokana na mti ule basi atalipwa kuwa ametenda wema mkubwa. (Bukhari).

- Dunia njema na ni yenye rangi ya kijani kibichi, na kwa hakika Mwenyezimungu amekufanya wewe (Mwanadamu) kuwa ni msimamizi/Mlinzi wake, na anamuona kila mmoja jisi anvyotekeleza jukumu hilo… (Muslim)

- Itumikie dunia yako kama kwamba utaishi milele na jiandae kwa ajili ya akhera yako kama kwamba utakufa kesho. Hadith Bukhari

- Hapana binadamu atakaeuwa kiumbe kidogo au kikubwa pasina kuwa na haki ya kufanya hivyo, basi Mwenyezimungu atamuuliza juu ya haki hiyo siku ya kiama. Maswahaba wa Mtume SAW walipomuuliza Mtume SAW juu ya maana ya kauli "pasi na kuwa na haki nacho" alijibu ya kuwa ni haki ya kuchinja na kukila wala siyo kukiua au kukikata kichwa na kukitupa. (Imesimuliwa na Ahmad, Al Nasai na Darimi na baadae (At Tirmidhi))

- Utakapoua ndege pasi na kuwa na shida nae, atashitaki siku ya kiama kwa kusema "ewe Mola wangu Mtu Fulani ameniua kwa ajili ya kufanya mchezo tu sio kwa ajili ya kunitumia. (Imesimuliwa na Al Nasai na Ibn Habban).

- Ataingia motoni mwanamke aliemfungia paka pasina kumpa chakula au kumwacha akatafute chakula mwenyewe (Al Bukhari).

- Mtume wa Mwenyezimungu (SAW) alikuwa akisafiri na kundi la masahaba wake akiwemo mwanamke wa Kiansaar aliekuwa akiendesha ngamia. Alipofika pahali fulani, yule ngamia alikataa kuendelea na safari, yule mwanamke alimlazimisha kuendelea, ndipo mtume SAW alipomwambia "usimlazimishe kuendelea na safari isipokuwa mtue hiyo mizigo uliyompakia na umwache kwanza aendelee pasina kuwa na mzigo. (Muslim).

- Itakapofika siku ya mwisho na mmoja wenu anao mche wa mti mkononi mwake ambao alikuwa anataka aupande basi na aupande, Mwenyezimungu atamlipa kutokana na jambo hilo. (Sunan al Bayhaqi al Kubra)

- Atakaeukata mti (mkubwa) kwa makusudi kwenye makaburi (pahala walipozikwa watu) ni mfano wa alievunja mlango wa Alkaba kwa mikono yake.

## VITABU REJEA


1. Bewley, Aisha, Glossary of Islamic Terms, Ta-Ha London, 1998.
2. Crump, Andy, Dictionary of Environment and Development, Earthscan London, 1991.
3. Dien, Mawil Izzi, Islam and Environmental Theory and Practice, Journal of beliefs & values no 1,1997, carfax, *http://www.lamp.ac.uk/trs/staffgale/mawil_paper.html*
4. Islam Set Web Journal, Environmental Protection in Islam, *http:www.islamset.com/env/html.*
5. Jode, Helen de, Misali Ethics Project, unpublished paper, Zanzibar, 2000.
6. Jumbe, Aboud, Freedom Guidance and Responsibility in Islam, Published in Zanzibar, 2001.
7. Khalid, Fazlun, Ilm ul Khalq (Knowledge of Creation), unpublished paper, 2002.
8. Khalid Fazlun, Islam and the Environment, Encyclopedia of Global Environmental Change, Vol.5. John Wiley and Sons, Chichester, 2002
9. Khalid, Fazlun, Misali Ethics Pilot Project, Consultants Report, 2001.
10. Khalid, Fazlun, Qur'an Creation and Conservation, IFEES, Birmingham, 1999.
11. Khalid, Fazlun and O'Brian Joan, Islam and Ecology, Cassell, London, 1990
12. Maamiry Ahmed Hamoud Al, Islam and Economic Prosperity in the Third World Countries, 1983.
13. Meadows, Donella H. Harvesting one hundreds fold, key concepts and case studies in Environmental education (UNDP), 1989.
14. Az-Zubaid, Al Imam Zain-ud-din Ahmad Abdul-Lateef, Sahih Bukhari Arabic English translation, Translated by Khan. Muhammad Muhsin, 1994
15. Samarrai Mawil Y. Izza Dean, Islamic Environmental Ethics, Law and Society, ….., 1990.
16. Sinha, Rajiv K., Environmentalism and Environmental Ethics in the Religious Faith and Philosophy of India, volume 15, number

2, 1994 pp 141-142.
17. UNEP, Cultural and Spiritual Values of Biodiversity, 1998.
18. Lieske Edward and Robert Myers, Coral reef fishes, 1994.
19. Fransis Julius, Stephen Mwinuka and Matthew Richmond, A school teacher's guide to environmental education in the Eastern African region, 2000.
20. Westmacott, S. Teleki, K. Wells, S.M. West, J. Management of bleached and severely damaged Coral reefs, 2000.

**Angalizo kuhusiana na marejeo ya tafsiri ya Qur'an iliyotumika.**

Qur'an inaaminika kuwa bado kuweza kutafsiriwa kikamilifu katika uhalisi wake kupitia lugha nyenginezo. Kwa maana hiyo, Mwenyezimungu ametujaalia kuchukua nukuu kutoka katika tafsiri mbali mbali za Qur'an ili kuweza kukaribisha na kuleta maana inayohitajika kwa ukaribu zaidi.

## KIARABU - KISWAHILI

**'Adl** –Uadilifu, utendaji wa mambo kwa kuzingatia haki na kipimo; bila upendeleo(usawa).
**'Alamin** –Ulimwengu wote na kila kilichomo, viumbe wote.
**Amanah** – dhamana; jukumu la kimaadili; wajibu ambao Mwenyezimungu amemwamuru mwanadamu kuutekeleza,.
**Ardh** – ulimwengu, ardhi, dunia.
**Aya** – sentesi ndani ya qur'an, dalili au ishara - ikimaanisha alama za uwezo wake Mwenyezimungu ambazo zipo katika dunia na ambazo mwanadamu anaziona.
**Din** – Mfumo au utaratibu wa maisha ambao mwanadamu amejiwekea kuufata.
**Fasad** – uharibifu, ubadhirifu.
**Fitra** – umbile asilia lililoumbiwa viumbe au dunia; maumbile ya mwanadamu katika kushikamana na maumbile.
**Halal** – kilichoruhusiwa na sheria ya kiislam kina thawabu kwa kutenda kwake.
**Haram** – kilichokatazwa na sheria ya Kiislamu na kina adhambi na adhabu ikiwa utakifanya.
**Haq** – Ukweli, uadilifu, usahihi.
**Imaan** – itikadi ya moyo, imani; kukubali kuwepo kwa Allah na mtume wake, malaika wake,vitabu vyake na siku ya mwisho.
**Ihsan** – Ukamilifu wa utiifu kwa Allah Ta'ala, kumuabudu Allah kama kwamba unamuona na ikiwa humuoni basi yeye anakuona.
**Islam** – kusalimu amri bele ya Allah, kujitolea nafsi au kuridhia kufanya ambayo anayataka Allah taala kufanywa kwa viumbe vyake vyote.
**Khaliq** – Muumba wa kila kitu.
**Khalq** – umbile /maumbile.
**Khalifa** – Kiongozi, msimamizi, mwenye kusimamia, aliekuja kurithi waliotangulia.
**Mizan** – uwiano; kipimo; alama ya mshikamano na kutegemeana katika mfumo wa maumbile.
**Muislam** – ambae anaefuata Uislam; yule mwenye kujitolea nafsi au kuridhia kufanya ambayo anayataka Allah taala yafanywe kwa viumbe vyake vyote.

**Musrifeen** – Wenye kufanya fujo katika kutumia, wasijali upotevu wa raslimali,waharibifu ndani ya dunia.
**Qis't** – haki; kipimo cha usahihi.
**Rak'a** – kifungu kimoja cha swala ndani ya swala kuanzia kisimamo hadi mwisho wa sujuda ya pili.
**Sala** – Swala tano za lazima kwa siku, ibada yenye mfumo maalum wa kusimama, rukuu, itidali, sijida, kitako huku ikiambatana na maneno maalum kwa ajili ya kumpwekesha na kumuomba Mwenyezimungu ambayo inatekelezwa mara tano kwa siku.
**Samawat** – Mbingu (saba) alizoumba Mwenyezimungu.
**Shahada** – Kukubali kwa moyo na kubainisha kwa ulimi kwamba hakuna Mola anaestahiki kuabudiwa kwa haki isipokuwa Allah an Muhammad ni Mjumbe wake.
**Shari'a** – Njia / mwelekeo wa kumdhibiti mwanadau ili kufanya aliyoamriwa na Allah.
**Sujud** – Kitendo cha kunyenyekea kwa viungo saba ikiwemo paji la uso mikono, magoti, vidole vya mguu na kadhalika, huku vikiwa vimegusa ardhi ndani ya swala au nje ya swala au maana nyengine ni kunyenyekea kwa utiifu.
**Sunna** – maneno na matendo yaliyofanywa au kupendezeshwa kufanywa na mtume ambayo yakifanywa na muislamu atalipwa thawabu na yasipofanywa hapatokuwa na malipo yoyote.
**Sura** – Sura, kifungu cha aya au maneno ndani ya Qur'ani.
**Taqwa** – Tendo la kuishi kwa kumuogopa Mwenyezimungu.
**Tawheed** – Mafundisho au imani ya kumuamini na kumpwekesha Mwenyezimuingu moja tu pasina kumshirikisha na kitu chengine.
**Wazan** – Kipimo, mizani.

## MISAMIATI MAARUFU INAYOTUMIKA KATIKA MASUALA YA UHIFADHI

**Bio-anuwai (Biodiversity)** – Hali ya kuwepo na kutofautiana kwa viumbe hai mbali mbali katika sehemu.

**Uhifadhi (Conservation)** – Kusimamia maliasilia bila ya kuziharibu raslimali ziliopo au Mazingira yake ikijumuisha kutunza na kutumia kwa uadilifu.

**Ekologia (Ecology)** – Somo la mahusiano ya viumbe hai na Mazingira yao na athari za mwanadamu katika Ulimwengu.

**Miundo ya kiekologia (Ecosystem)** – neno la kisayansi linalotumika kuonesha mshikamano na tofauti kwa jamii ya viumbe na Mazingira yao.

**Aina zilizo hatarini kutoweka (Endangered species)** – wanyama au miti ambayo imetajwa na wataalamu kuelekea kutoweka au kupotea ikiwa hatua madhubuti hazitochukuliwa.

**Mazingira (Environment)** – Neno linalojumuisha vitu au maumbile asilia ikiwemo bahari, ardhi, anga pamoja na kila kilichomo ndani yake.

**(Habitat)** – Vitu vinavyomzunguuka mwanadamu kimaumbile ambapo kutokana na harakati zake anaweza kuathirika kwa namna moja au nyengine, hii inajumuisha hata harakati za kiuchumi, kijamii na kisiasa.

**Makazi (Holistic)** – sehemu au mazingira yanayoonekana kwa ajili ya maisha za wanyama, miti au hata binadamu.

**Maliasili (Natural resources)** – sehemu ya utajiri asilia katika ulimwengu ikiwemo ardhi, bahari, misitu, hewa, vyanzo vya maji na kadhalika ambavyo vinasaidia maisha ya mwanadamu au vinaweza kuwa ni chanzo cha uchumi au utajiri; wa taifa.









